# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

### Kikao cha Tano – Tarehe 6 Septemba, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Nne na leo ni Kikao cha Tano. Katibu

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA - MHE. PASCHAL P. KATAMBI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendments) Bill, 2021).*

**SPIKA:** Ahsante Naibu Waziri - Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi. Sasa naomba nikuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendments) Bill, 2021).*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti Mheshimiwa Ramadhan Ighondo, Mjumbe wa Kamati. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali la kwanza la Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mbunge wa Pangawe. Mheshimiwa Haji uliza swali lako sasa.

Na. 54

### Mawakala wa Ajira Nchini

**MHE. HAJI AMOUR HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeruhusu uwepo wa Mawakala wa Ajira nchini:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani juu ya ajira za nje ya nchi kwa Vijana wetu?

(b) Je, ni upi mchango wa Mawakala wa ajira hapa nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mbunge wa Pangawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwasadia vijana wetu kupata ajira za nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kubaini nchi za kimkakati zenye fursa za ajira za staha na kuingia makubaliano *(bilateral agreement)* na nchi husika; kuwajengea uwezo vijana wa Kitanzania kuwa na ujuzi utakaowawezesha kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi; na kujenga mfumo wa huduma za ajira ambao pamoja na mambo mengine utarahisisha utafutaji wa kazi nje ya nchi; kuweka mwongozo wa kuratibu shughuli za wakala binafsi wa huduma za ajira wanaopeleka watu nje ya nchi; na kufanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Ajira ya mwaka 1999 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2014 ili kuweza kuendana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Juni, 2021 Mawakala wa ajira nchini wamechangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya vijana 39,273 wamepewa huduma ya ushauri nasaha *(employment and career counseling).* Aidha, vijana 19,509 wamepewa mafunzo ya watafutakazi, vijana 11,371 wameunganishwa na fursa za mafunzo ya utarajali na vijana 10,554 wameunganishwa na fursa za kazi ndani na nje ya nchi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Pangawe.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina maswali yangu ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Je, Serikali haioni haja ya uwepo wa Sera ya Uwakala wa Ajira pamoja na miongozo sahihi kwa Balozi zetu juu ya vijana wetu wanaokwenda kufanya kazi katika nchi hizo?

Mheshimiwa Spika, la pili: Je, kuna ushirikiano gani kati ya Wizara inayoshughulikia ajira ya hapa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Haji Amour Haji, kwa kuwa swali lako umelisoma, basi sitaliruhusu. Tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kwa niaba yake.

Na. 55

**Serikali Kutekeleza Ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI K.n.y. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya shilingi milioni 400 aliyoahidi Waziri Mkuu kuchangia katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasekese kinachojengwa na wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha utoaji wa huduma za afya ya msingi kwa wananchi ikiwemo upatikanaji wa huduma za upasuaji. Ujenzi na ukarabati huo unahusisha pia utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Serikali kuchangia shilingi milioni 400 ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kasekese imetekelezwa, ambapo fedha hizo zimepelekwa kwenye Kata ya Kasekese tarehe 25/8/2021 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, majengo manne yanatarajiwa kujengwa, ambayo ni jengo la wodi ya wazazi, jengo la upasuaji, jengo la kufulia nguo na nyumba ya mtumishi. Aidha, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje la Kituo cha Afya Kasekese umekamilika kwa gharama ya shilingi 164.9 kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Awali ya yote naishukuru Serikali kwa kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Maswali yangu madogo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Ikola wamefanya kazi nzuri ya ujenzi wa Hospitali Teule: Nini kauli ya Serikali katika kuwaunga mkono wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Awamu ya tatu na ya nne kwa maana ya upelekaji vifaatiba katika vituo vya afya, tunacho Kituo cha Afya cha Ilembo, kwa bahati mbaya

hakikubahatika kupata fedha hizo: Nini kauli ya Serikali katika kupeleka vifaatiba?

**SPIKA:** Majibu ya maswali ya Mheshimiwa Kapufi, Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana kwa kupongeza juhudi za Serikali za kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya, lakini hizi kazi zote zinazofanywa ni dhamira ya Serikali hii ya Awamu ya Sita na Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kule walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kata hii ya Ikona ambayo wananchi wamechangia nguvu zao kujenga kituo cha afya, kwanza niwapongeze sana kwa kuchangia nguvu zao, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge pia kwa kuhamasisha wananchi hawa, lakini nimhakikishie kwamba Serikali inaendelea na mipango yake ya kuchangia nguvu za wananchi kwa kupeleka fedha ili kukamilisha vituo vya afya ambavyo tayari wananchi wameanza na ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hii itawekwa kwenye mipango na kadri ambavyo tutapata fedha tutakwenda kuhakikisha kwamba kituo hiki pia kinasaidiwa ili kikamilike na kuanza kutoa huduma bora za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Ilembo nayo kuhusiana na vifaatiba, tumeweka mkakati na katika mwaka huu wa fedha tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 100 zinazotokana na tozo kwa ajili ya vifaatiba katika vituo

vyetu. Kwa hiyo, tutaenda kuhakikisha vituo kama hivi pia vinapata fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutampa kipaumbele katika kituo hicho. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi ya Serikali ya ujenzi wa vituo vya afya vilevile ni kupandisha hadhi vituo vya afya kuwa Hospitali za Wilaya. Hospitali ya Manyamanyama ni hitaji la Halmashauri ya Bunda kuwa Hospitali ya Wilaya. Hili swali nimeuliza huu ni mwaka wa 11; na liliamuliwa tangu enzi ya Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, Mheshimiwa Mwakyusa, mpaka leo wameweka kibao cha Hospitali ya Wilaya, lakini vifaatiba na madawa mnatoa mgao wa kituo cha afya:-

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali hii itaipa Hospitali ya Manyamanyama mgao wa vifaatiba na madawa kama Hospitali ya Wilaya na siyo tena kituo cha afya, maana kinatoa huduma mpaka katika Wilaya za jirani? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupandisha vituo vya afya kuwa hospitali una vigezo kadhaa ambavyo vimewekwa. Moja ni kuwa na Halmashauri ambayo haina

Hospitali ya Wilaya ndipo kituo kimojawapo cha afya ambacho kinakidhi sifa, kinapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Halmashauri. Kwa mfumo, sera na miongozo ya sasa,

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ipo moja tu katika Halmashauri. Kwa hiyo, kwa sababu Halmashauri ya Mji wa Bunda ina Hospitali ya Halmashauri; na hiki kituo cha afya kwa *nature* yake kinahudumia wananchi wengi, tutahakikisha tunaongeza mgao wa dawa na vifaatiba ili iweze kuendana na idadi ya wananchi wanaopata huduma pale wakati tunaendelea kuboresha Hospitali hii ya Wilaya iliyopo katika Halmashauri ya Bunda. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Jambo moja tu Mheshimiwa Naibu Waziri, mnaweza mkaangalia kwenye Wizara, katika yale maagizo ya majengo yanayojengwa kwenye kituo cha afya, sisikii ile *theatre* ndogo ikitajwa. Kwa sababu lengo mojawapo la vituo vya afya hasa ni ili wamama wajawazito na wenyewe waweze kufanyiwa huduma pale, lakini maelekezo yenu *theatre* haimo.

Sasa kama haimo, ile shida ya kutatua hilo tatizo bado ipo pale pale. Nafikiri ni vizuri kuona namna gani haka ka-*theatre* nako kakawa katika hiyo *package. (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimepokea.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Conchester Leonce Rwamlaza, bado tupo TAMISEMI.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wenye viwanja katika Kata ya Mkonze Miganga West na East na sehemu nyinginezo katika Jiji la Dodoma ambako kunapitwa miradi ya kimikakati, naomba sasa swali lao Na. 56 lipate majibu. *(Makofi)*

Na. 56

**Fidia kwa Wananchi Wenye Maeneo *Miganga West*na *East* – Jiji la Dodoma**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wenye Viwanja eneo la Miganga *West* na *East,* Kata ya Mkonze katika Manispaa ya Jiji la Dodoma kwa kuwa uthamini ulishafanywa na baadhi ya Wananchi bado hawajalipwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Miganga *West* na *East* katika Kata ya Mkonze ni miongoni mwa maeneo ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambayo yamepangwa, kupimwa viwanja na kumilikishwa kwa wananchi ili waviendeleze kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Mji Mkuu *(Master Plan).*

Mheshimiwa Spika, kufuatia uwepo wa miradi ya kimkakati wa ujenzi wa reli ya kisasa *(SGR)* na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa 400*KV* kutoka Chalinze hadi Zuzu inayotekelezwa na Serikali kupita katika eneo hili na kuathiri viwanja vilivyomilikishwa, imelazimu eneo hilo kutwaliwa chini ya Sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya Mwaka 1967, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, Kanuni za Ardhi za Mwaka 2001, Miongozo ya Uthamini na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya uthamini kwenye jumla ya viwanja 309 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.77 vilivyoathiriwa na mradi wa reli ya kisasa ambapo kiasi cha shilingi milioni 576.5 imeshalipwa kwa wananchi ikiwa ni fidia ya viwanja 231. Viwaja 78 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.2 vinaendelea kuhakikiwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu ili kukamilisha taratibu za fidia zao kwa mujibu wa sheria. Aidha, Serikali imeshafanya uthamini kwenye viwanja 123 na makaburi manne vyenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 1.1 vilivyoathiriwa na mradi wa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa 400*KV*.

Mheshimiwa Spika, wananchi ambao viwanja vyao vimeathirika na mradi huo, watalipwa fidia mara baada ya Mthamini Mkuu kukamilisha taratibu za kisheria. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kitu cha kwanza, majibu niliyopewa ni tofauti kabisa na majibu ambayo nimesomewa na Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sheria inasema, wakithamini wanapaswa walipe wale wathaminiwa ndani ya miezi sita; na kwa kuwa watu wengine wameshalipwa: Je, wale ambao hawajalipwa, kuna nyongeza yoyote ambayo itawekwa kwa ajili ya fidia kwa sababu Serikali imechelewa kulipa na hawajaweza kuendeleza maeneo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: mwananchi yeyote anapochukua kiwanja cha Serikali ambacho kimepimwa anakuwa amejihakikishia makazi yake kwa sababu atajiandaa katika maisha yake; kuchukua viwanja vyao, ukachelewa kulipa ni kuwadumaza: Pamoja na majibu aliyotoa, wale watu waliobaki watalipwa lini kwa *commitment* ya Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri Ardhi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Conchesta kama alivyouliza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dugange kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ana hofu ya kujua kwamba wale ambao hawajalipwa, watalipwaje pesa zao? Je, kutakuwa na nyongeza? Sheria iko wazi na tuliipitisha hapa 2019 tukafanya marekebisho kwamba inapofika miezi sita kama hajalipwa, tunaanza ku-*calculate interest* kwa bei ya soko iliyopo wakati huo. Hii inakwenda ndani ya miaka miwili, ikifika miaka miwili hawajalipwa maana yake lile zoezi inabidi lianze tena uthamini upya. Sheria tuliipitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu tu kwamba watu hawa watalipwa kwa bei ya soko wakiwa wamewekewa na riba yao katika pesa walizochukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anauliza, ni lini pengine wataacha kuchukua maeneo ya watu halafu wanakuwa hawana uhakika wa malipo yao? Naomba niseme tu kwamba katika maeneo ambayo Serikali inakuwa na *interest* nayo, lazima itaongea na washirika waliopo pale, wenye ardhi zao, kuwaambia dhamira na nia njema ya Serikali; na kabla ya kutwaa kunakuwa na makubaliano ambayo ni lini maeneo haya yatatwaliwa na kwa kazi ipi? Inapokuwa na *public interest,* huwa haina majadiliano zaidi ya kukaa nao na kukubaliana nini kifanyike?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hili ambalo tayari tunaona ni miradi mikubwa ya Kiserikali ambayo inapita, hatutakuwa na mjadala mwingine isipokuwa ni kuzungumza nao. Tayari Tume ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika maeneo yote inayopita miradi mikubwa,

wameshaandaa mpango wa matumizi ya ardhi. Kwa hiyo, wale watakaobaki pale, watapimiwa maeneo yao, wale watakaotakiwa kuondoka kwa ajili ya kupisha pengine labda ni zile *stations* zinazojengwa, basi watapewa fidia yao kwa mujibu wa soko la wakati huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali sasa la Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, uliza swali lako tafadhali. *(Makofi)*

Na. 57

**Ulinzi wa Watoto Dhidi ya Vitendo Viovu**

**MHE. SALMA R. KIKWETE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wazazi na Walezi wanatoa ushirikiano katika kuwatetea na kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ubakaji, ulawiti na unyanyasaji unaoendelea kwa sasa?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Afya, mwenyewe majibu tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete Mbunge wa Mchinga kama kwamba je Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wazazi na na walezi wanatoa ushirikiano katika kuwatetea na kuwalinda watoto dhidi ya ubakaji, ulawiti na unyanyasaji unaoendelea kwa sasa?

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali hili kama ifuatavyo; katika kukabiliana na tatizo la Ubakaji, Ulawiti na Unyanyasaji wa watoto, Serikali imechukua hatua zifuatazo: Kuandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA wa mwaka 2017/2018 -2021/2022) ambapo kupitia Mpango huu Serikali imekuwa ikitekeleza afua zinazolenga Kutoa Elimu ya Malezi ya watoto

kwa wazazi/walezi; Kutoa msaada wa Kifamilia na Mahusiano; na Kusambaza *Agenda* ya Taifa ya Wajibu wa Wazazi/Walezi katika malezi chanya ya familia.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na; Kuandaa programu ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya awali ya mtoto, kupitia *program* hii vituo vya majaribio 30 vya kijamii vya malezi, makuzi, na maendeleo ya awali ya mtoto vimejengwa katika mikoa miwili ya Dar es Salaam ambapo ni vituo 10 na Mkoa wa Dodoma vituo 20 na Serikali inaendelea kuhamasisha ujenzi wa vituo vingine katika mikoa iliyobaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kikwete uliza swali tafadhali.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Tunajua na tunakumbuka kwamba malezi bora ya mtoto yanaanzia katika umri mdogo na ili mtoto aweze kukua anahitaji malezi rafiki kutoka kwa wazazi na walezi.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba watoto hawa wanalelewa na hawa wazazi na walezi yanapowakuta mazingira mabaya mtoto anapoeleza kwa wazazi au walezi anatishwa na wakati mwingine wanaofanya vitendo hivyo wapo ndani ya familia hiyo hiyo, aidha inaweza ikawa ni mjomba, ndugu wa karibu, dada anaogopa kueleza tatizo matokeo yake mtoto anaumia na anaharibika sana kisaikolojia.

Je, Serikali hapa inatuambia nini? Na sababu kubwa ni mojawapo Tanzania ina utaratibu mzuri sana juu ya mpango wake kuna Jirani, kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, kuna Kitongoji kila mtu linapotokea kila mtu analijua. Serikali mnatuambia nini juu ya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili mmeeleza kwamba kuna mkakati ambao unamalizika, kuna MTAKUWWA, unaomalizika 2022 lakini kuna *program* ambayo imeandaliwa

na mpaka sasa kuna vituo 30, vituo 10 vipo Dar es Salaam, vituo 20 viko Dodoma. Nini matokeo ya vituo hivi ambavyo ni vituo vya majaribio? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Afya Dkt. Doroth Gwajima tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana namshukuru Mheshimiwa Salma Kikwete Mbunge wa Mchinga kwa maswali yake mazuri ya nyongeza na nashukuru sana ni kama ametoa semina hapa. Ni kweli katika swali lake la kwanza masuala ya walezi yanaanza tangu mtoto akiwa mdogo pia matatizo anayopata mtoto akiwa mdogo yanatokana na ile jamii anayoishi nayo ndani na ndivyo tafiti zinavyoonyesha kwamba athari ya kwanza ni wale ambao wanaomzunguka yule mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika kulifanyia kazi hili Serikali tumejipanga kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii yetu na Maendeleo ya Jamii hivi sasa tunakwenda kuanzisha mpango kama tunavyofanya kwenye afya, huduma za mkoba au *mobile* kuzifikia hizi familia na kuzielimisha kaya kwa kaya kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mwenyewe juzi nilitoka Mwanza kama mwezi mmoja umepita nilifika mpaka kwenye nyumba ambako mtoto aliketishwa anamuhudumia bibi haendi shule mpaka amefika miaka 9 nikajifunza mambo mengi. Kwa hiyo, tukaona kwamba tunavyowafikia wagonjwa wanaoumwa kwa *mobile* na kliniki tuanzishe hiyo kwenye maendeleo ya jamii ili tuguse kabisa hizi jamii na kuanza kuwalea wazazi wenyewe ili waje kuwalea watoto wote wakiwa na *confidence* moja.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya vituo hivi vya Dodoma na Dar es Salaam naomba nilipokee hili tumeshaanza *evaluation* kwa ajili ya kwenda kuona ile *impact* tuwasilishe taarifa kwenye kamati yetu na itakuja kufika Bungeni kwa ridhaa ya Spika *then* tunakwenda

kupeleka nchi nzima, faida ni kubwa kuliko kutokuwa na vituo hivyo.

**SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufika kwa Mwanza kwa yule binti wa miaka 9 na tunakushukuru kwa hatua ambazo mmezichukua ni *story* inayosikitisha sana. Tunakwenda Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Ahmed Ally Salum Mbunge wa Solwa.

Na. 58

**Kukamilisha Ujenzi Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Isholo – Wilaya ya Shinyanga**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa skimu ya Umwagiliaji iliyopo Kata ya Isholo, Wilayani Shinyanga utakamilika baada ya kusimama tangu mwaka 2014?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum Mbunge wa Jimbo la Solwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo chini ya Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* kupitia Mpango wa Kuendeleza Kilimo Wilayani *(DASIP)* ambao ulianza mwaka 2006 na kumalizika Disemba, 2014 umejenga skimu mbalimbali za umwagiliaji ikiwemo mradi wa umwagiliaji Ishololo. Kazi zilizokuwa zimefanyika katika mradi wa Umwagiliaji Isholo ni ujenzi wa tuta la bwawa ambao ulifikia asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mradi huu kuwa miongoni mwa miradi ambayo haikukamilika chini ya

mpango tajwa kufuatia fedha iliyotengwa kutotosha kumaliza kazi zote, katika mwaka 2016, baada ya Wizara kupitia upya Mpango Kabambe wa Umwagiliaji, mradi huu umepangwa katika vipaumbele na umebainisha njia nzuri ya kumalizia ujenzi wa skimu ya Ishololo.

Mheshimiwa spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuendeleza ujenzi wa skimu hii katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(FYDP 2020-2025).* Aidha, Tume inaendelea kutafuta fedha kutoka Vyanzo mbalimbali vya Fedha ili kukamilisha ujenzi wa mradi huo katika mwaka wa fedha 2021/2022 na hivyo kuwawezesha wakulima wa Ishololo kunufaika na skimu hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ahmed Salum.

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana yanayopendeza kuhusu Bwawa la Ishololo. Lakini kwa kuwa tayari andiko lilishafanyika kwa maagizo yake mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri mwezi nne liko mezani kwake na kwa kuwa mradi huu umechukua muda mrefu na ni muhimu sana kwenye Kata ya Usule Kijiji cha UsholOlo na kwa kuwa tayari hapo ameonyesha *commitment* kwamba 2021/2022 inaweza likajengwa sasa bwawa hili na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ikiendelea kutafuta fedha.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba katika mradi huu uwe ni mradi wa kwanza kabisa pale ambapo Tume itakapopata fedha katika mwaka 2021/2022?

Mheshimiwa Spika, swali lingine ningependa sana Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kutembelea bwawa hili tukienda pamoja ili kuweza kutoa matumaini mapya kwa wananchi wa Kijiji cha Ishololo na Kata ya Usule?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mhehsimiwa Naibu Waziri wa Kilimo tafadhali, Mheshimiwa Hussein Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Ahmed Mbunge wa Solwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwenda kutembelea katika eneo la Ishololo nataka tu nimwahidi kwamba niko tayari na tutakwenda Pamoja. Pili nataka tu nimhakikishie kwamba mradi wa Ishololo, Mradi wa Nyida ambao mradi huu unahusisha vile vile Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Nzega *District Council* kwa maana ya ambayo inahudumia majimbo 3, jimbo la kwake, jimbo la Mheshimiwa Kigwangala na Mheshimiwa Selemani Zedi. Nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba ni miongoni mwa miradi ya *priority* katika Wizara katika mwaka huu wa fedha na tumeshaanza kufanya *visibility study* na tutatumia wataalamu wetu wa ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii fedha ikipatikana.

**SPIKA:** Ahsante sana tunahamia kwa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo bado tuko kilimo

Na. 59

**Makampuni Wazawa Kuwezeshwa Kuwalipa Wakulima wa Tumbaku Wanaponunua Tumbaku**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha kampuni za wazawa ili ziwalipe wakulima mara wanaponunua Tumbaku?

(b) Suala la kupata wanunuzi zaidi wa kununua tumbaku ni la muda mrefu; je kuna mafanikio yaliyopatikana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo bado tuko kwako.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Jimbo la Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu biashara ya tumbaku imekuwa ikiendeshwa bila kampuni za kizawa kushiriki katika biashara ya Tumbaku na kampuni za nje pekee ndizo zilikua zinashiriki katika biashara ya tumbaku. Wakati wa ununuzi wa tumbaku kupitia kampuni za nje ununuzi wa tumbaku ulishuka hadi kufikia tani 42,000 za mkataba na baada ya kampuni za wazawa kuingia katika ununuzi wa uzalishaji umeongeza kufikia tani 68,571 za tumbaku kupitia kilimo cha mkataba. Katika masoko ya tumbaku ya msimu wa kilimo 2020/2021 jumla ya kampuni tisa zinanunua tumbaku ya wakulima zikiwemo kampuni saba za wazawa. Hata hivyo, Kampuni hizo zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kupata mitaji ya kutosha hali inayosabisha kuchelewa kuwalipa baadhi ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hiyo, Mwezi Mei, 2021 Wizara ya Kilimo ilikutanisha kampuni za wazawa na taasisi za fedha kwa lengo la kukubaliana masharti nafuu yatakayowezesha kampuni hizo kupata mikopo kwa riba nafuu. Mafanikio ya majadiliano hayo yameanza kupatikana ambapo benki ya *CRDB* imeridhia kuzikopesha kampuni mbili za *Mo Green International* na *Magefa Growers Limited*. Aidha, Serikali inaendelea kushirikiana na kampuni za ununuzi wa tumbaku na taasisi za fedha katika kutatua changamoto ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta soko la tumbaku katika nchi mbalimbali hasa nchi za Uarabuni, Afrika na Ulaya. Katika msimu 2020/2021 nchi yetu imefanikiwa kupata masoko mapya kwa kuuza tumbaku kwa majaribio katika nchi ya Romania, Poland na Uturuki. Aidha, sampuli za tumbaku zimetumwa nchini China na Korea Kusini kwa ajili ya masoko hayo. Juhudi za kuirejesha kampuni ya *TLTC* zinaendelea na mwishoni mwa mwezi Septemba 2021 Wizara itakutana uongozi wa kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kama nchi kuendelea kulea makampuni ya wazawa ili yawe na uwezo wa kununua tumbaku kama makampuni ya kigeni yanavyounganisha na taasisi za fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Sitta tafadhali uliza swali lako.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niongee kwa uchungu. Wakulima wameuza tumbaku tangu mwezi wa tano mpaka sasa hawajalipwa na wao wanategemea tumbaku ndio waweze kuishi. *AMCOS* zifuatazo naongea kwa uchungu, *AMCA*, *MISSION*, MTAKUJA, IFUTA, TUNAWEZA, KASISI, KATUNGURU, SIPUNGU, MISANGI, KALEMBERA, BLOKU, JIKOMBOE na UPENDO hawajalipwa hela tangu mwezi wa tano naongea kwa uchungu waishije na sisi tunasema wakulima wanategema kilimo. Lini Serikali itawalipa hawa wakulima ili nao waweze kuendesha maisha yao?

Mheshimiwa Spika, la pili wakati huo bei ya mbolea imefikia hadi laki moja karibu wataanza kutengeneza mabero yao wanafanya nini, hawajalipwa halafu bei ya mbolea imefika mpaka laki moja, naongea kwa uchungu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri yuko mbali angekuwa karibu nina hakika angezabwa kibao. Majibu ya uhakika kwa Mheshimiwa Mbunge wa Urambo kwa maswali yake ya uchungu kabisa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpe pole na nimwambie kwamba kama Serikali tunakiri uwepo wa changamoto hii. La pili ambalo ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakafahamu na yeye ni mmoja kati ya Wabunge ambao mwaka 2019 aliomba Serikali ifanye juhudi za kuhakikisha *AMCOS* alizozitaja na baadhi ya *AMCOS* katika Mkoa wa Tabora ambazo hazikuwa na mikataba na

ziliachwa na *TLTC* na ziliachwa na jumla ya tani 12000 ya tumbaku ambazo hazikuwa na wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hawa wa kitanzania ndio walio-*rescue sector* hii na leo tuko *confident* bei ya tumbaku imetoka dola 1.4 mpaka dola 1.65, zipo changamoto za kuchelewa kulipwa malipo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na niwahakikishie wakulima wa tumbaku moja tutawahakikishia kwamba waliofanya masoko ya mwezi Mei, Juni na Julai tutahakikisha kwamba malipo yao yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, la pili tumebadili mfumo wa uuzaji baada ya matokeo ya mwaka jana kwamba makampuni haya sasa tumbaku yao yote wanayochukua kwa wanunuzi haziondoki ndani ya mipaka ya nchi yetu mpaka fedha zimepatikana. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba hizi changamoto tutaendelea kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei na kuhusu pembejeo sasa hivi wakulima wa tumbaku tumeshaanza kuwapelekea mbole za mabedi bila wao kulipa hata shilingi. Tumetengeneza utaratibu wa *suppliers* wanapeleka na watalipwa mwisho wa msimu kwa hiyo nataka nimhakikishie kwamba pembejeo zimekwenda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupanda kwa bei ya mbolea ni jambo ambalo limetokea na ni kweli nani suala la kidunia. Hatua tuliyochukua mwezi uliopita tumeenda ku-*review* bei ya tumbaku na wanunuzi wote na kuifikisha dola 1.65 tuki-*accommodate* ongezeko la bei ya mbolea ili wakulima hawa wasiweze kupata hasara. Nimhakikishie mama Sitta na niwahakikishie wakulima wa tumbaku tumeanza mazungumzo na taasisi za fedha tutahakikisha msimu ujao changamoto ya *delay* ya *payment* inakwisha katika sekta ya tumbaku na tutafata sheria ambapo *credit facility* ni siku 14 na sekta hii iweze kuwa *stable.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa Mjumbe wa zamani wa Bodi ya Tumbaku.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii niwaulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakulima wa tumbaku wanalipwa *District SES* pia wanalipa tozo ile ya Vyama Vikuu vya Ushirika na Chama cha Msingi. Lakini imesikika mwaka huu pia kwamba wakulima wa tumbaku watakatwa na *TRA* kodi katika mauzo yao ya tumbaku. Nataka kujua Serikali suala hili ni kweli au siyo kweli?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi kabisa ni kweli au siyo kweli Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa. Ni kweli Bunge lako tukufu lilipitisha utekelezaji wa Sheria ya *Withholding Tax* ya 2% kwenye mazao ya kilimo. Lakini kama wizara hatua tuliyochukua kwamba mjengeko wa bei ya tumbaku huamuliwa kati ya mwezi wa pili, tatu na wa nne.

Mheshimiwa Spika, wakati mjengeko wa bei ya mauzo ya mwaka huu yamepitishwa suala la *withholding tax* halikuwepo. Kama Wizara tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha tumewaandikia ili tuone namna gani utekelezaji wa sheria hii uweze kuwa *withhold* kwa sababu mjengeko wa bei haukuhusisha *withholding tax* ya 2%. Jambo hili liko katika mazungumzo na wenzetu wa Wizara ya Fedha niwahakikishie tu kwamba tutafikia muafaka na kuweza kulinda maslahi ya wakulima katika eneo hili.

**SPIKA:** Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti mnapaswa kuwa makini sana katika kazi zenu, kwa sababu mambo yakifika hapa sisi tunaiamini kamati, mkiendelea hivi nitaifumua hiyo Kamati ya Bajeti.

Tumeweka watu tunaowaamini sana mle kwenye kamati ile lakini kama mnakwenda kule mnalalalala na kupitisha tu vitu kienyejienyeji mnatuponza. Mnapitishaje kitu kama hiyo bwana! Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan.

Na. 60

**Ujenzi wa Barabara ya Masasi Hadi Liwale kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza Ujenzi wa barabara ya Masasi hadi Liwale kupitia Nachingwea kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Geofrey Kasekenya Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Masasi hadi Liwale kupitia Nachingwea kwa kiwango cha lami ambapo kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya Masasi – Nachingwea – Nanganga yenye urefu wa kilometa 90 ilikamilika mwaka 2014 na sehemu ya Liwale – Nachingwea yenye urefu wa kilometa 130 imekamilika mwezi Juni, 2021. Katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 1,500 yaani sawa na shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Masasi – Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili kuhakikisha inaendelea kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka huu wa fedha wa 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 634 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pathan swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Katika hali halisi hiyo pesa iliyotengwa 1.5 kwa ujenzi wa barabara ya lami ni ndogo sana na upembuzi yakinifu umefanyika muda mrefu sana.

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza pesa angalau hata kidogo, watutengenezee hata kilometa 30 tu, kwa mwaka huu, halafu na zile zitakazobakia waongoze pesa kwa mwaka ujao watutengenezee? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli hela iliyotengwa ni hela ndogo kulingana na urefu wa barabara, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii fedha iliyotengewa ni fedha ya awali kwa ajili ya *mobilization* na kadri fedha itakavyoendelea kupatikana kwa jinsi Serikali itakavyopata, itazidi kuongezewa ili kujengwa kwa kiwango chote.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii inatakiwa ijengwe katika kipindi cha awamu yote hii ya miaka mitano. Kwa hiyo, kadri fedha itakavyoendelea kupatikana basi barabara hii tunahakika kwamba itajengwa yote kwa kiwango cha lami, kwa maana ya Masasi, Nachingwea hadi Liwale. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sijui kama umeshapita barabara ile ya Masasi, Nachingwea na Liwale, lakini kuna maeneo kati ya Nachingwea na Liwale, mvua hata ikinyesha, yaani hata ikinyesha mvua ya dakika tano magari yanakwama. Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, tafadhali uliza swali. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hii barabara siyo kwamba fedha Serikali hawana ya kujenga, ninachokiona hapa ni kwamba Serikali bado haijaamua kujenga hii barabara, kwa sababu zipo barabara zimefanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2018, mwaka 2017, mwaka 2016 zimeshajengwa na zingine zinajengwa. Lakini hii tangu mwaka 2014, ninaiomba Serikali iamue kwa maksudi kabisa kuikomboa Wilaya ya Liwale na Wilaya ya Nachingwea ili iweze kufunguka nasi kiuchumi tuweze kuwa miongoni mwa watu waliopo duniani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja ya vitu ambavyo vinaongoza katika kutengeneza hizi barabara kwa kweli ni uwezo wa Serikali kwa maana ya bajeti, lakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ahadi za viongozi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nachingwea - Liwale kwenye Ilani yetu ni kati ya barabara ambazo zipo kwenye usawa wa kilometa 7,500 ambazo zinatakiwa zikamilishwe usanifu wa kina kazi ambayo tayari imefanyika. Kwa hiyo ni hatua ya awali ambayo imefanyika na sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, usanifu tayari umekamilika kama ilivyoahidiwa kwenye bajeti mwezi Juni mwaka huu. Kwa hiyo, tayari Serikali imeshapiga hatua na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Liwale kwamba kwa kuwa tayari tumeshaanza kadri fedha zitakapopatikana naamini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe bado tupo kwenye swali hilo hilo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Kuchauka ameonesha masikitiko yake makubwa kabisa, naamini nasi umetupa nafasi kwa maana ya Wabunge wa Nachingwea, Ndanda, Masasi na maeneo mengine kwenye umuhimu wa hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nimuulize Mheshimiwa Waziri, Wizara imetenga shilingi bilioni 1.5 tu, kwa makisio ya sasa ni kama kilometa moja na nusu, wanapotaka kuanza kujenga barabara hii wataanzia kujenga upande gani? kwa sababu shida ipo Masasi, shida ipo pia Nachingwea. Watueleze wanataka kuanza kujenga upande gani kwa pesa kidogo namna hiyo waliyoitenga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mtihani huo, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Unaanzia Masasi, Nachingwea au Liwale penyewe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara tunachojenga ni kilometa hizo 45 kati ya Masasi na Nachingwea. Lakini hata ukianza Masasi, ukianza Nachingwea bado barabara ni ileile mtu atakapopita, atapita kokote. Nadhani nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la kuanza wapi ama wapi nadhani isingekuwa ni hoja kubwa cha msingi tukamilishe hizo kilometa 45 kwa sababu hata kama itaanzia Masasi, itaanzia Nachingwea, lakini atakayepita, atapita tu kwenye hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, nadhani hilo aiachie Wizara na wataalam wataangalia pia wapi tunapofanya *mobilization*

inaweza kuwa ni rahisi, jambo la msingi tukamilishe hizo kilometa 45. Ahsante.

**SPIKA:** Basi mkaanzie Liwale. Mheshimiwa Massare nimekuona kule Msekwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo kule Liwale, Nachingwea yanafanana kabisa na yaliyopo katika Jimbo la Manyoni Magharibi Mkoa wa Singida kuunganishwa na Mkoa wa Mbeya kwa barabara inayotoka Mkiwa, Itigi hadi Rungwa.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii?

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali hilo muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Massare Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba katika bajeti tuliyopitisha barabara hii ya kuanzia Mkiwa kwenda Rungwa, Lupa hadi Makongorosi, imetengewa bajeti kuanza kwa kiwango cha lami. Na sisi kama Wizara tunategemea muda wowote barabara hii iweze kutangazwa kwa ajili ya ujenzi, kwa sababu ni kati ya barabara chache ambazo zimebaki ambazo ni barabara kuu, *trunk,* yaani kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zote za manunuzi zimeshakamilika, tunachosubiri ni kutangaza hiyo *tender* kwa

sababu fedha imeshapitishwa na Bunge lililopita kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuhamie Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Waheshimiwa Wabunge, najua yapo maswali mengi sana ya barabara lakini tuvumiliane. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi uliza swali lako. Mheshimiwa Mariam.

Na. 61

**Mtaala Mmoja wa Elimu Tanzania Bara na Zanzibar**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuwa na Mtaala mmoja kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne kati ya Tanzania Bara na Zanzibar? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikishirikiana vizuri na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika masuala mbalimbali ikiwemo suala la elimu hususan katika utekelezaji wa mitaala na kutoa elimu bora kwa watoto wa kitanzania.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mitaala ya elimu kati ya Tanzania Bara na Visiwani, pande zote mbili hutumia mtaala mmoja kuanzia Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Sita. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam umeridhika.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja dogo la nyongeza:

Mheshimiwa Spika, kwa vile sasa Wizara ipo kwenye mchakato wa kukusanya maoni ya kurekebisha mtaala. Je, Serikali haioni sasa kuwa ipo haja ya kuweka mtaala mmoja wa elimu ya msingi kati ya Tanzania Bara na Zanzibar? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam nakupa nafasi tena, sasa uulize swali lako ukiniangalia, usipige chabo. *(Kicheko)*

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali sasa ipo kwenye mchakato wa marekebisho ya mtaala. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja sasa ya kuweka mtaala mmoja wa elimu kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Bara? *(Makofi/ Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa upande wa Elimu ya Msingi kuna tofauti ya mitaala kati ya Tanzania Bara na Visiwani. Kwa sababu kwa upande wa Tanzania Bara tunawapeleka watoto shule miaka saba kwa upande wa shule za msingi, lakini kwa wenzetu wa Tanzania Zanzibar wao wanakwenda kwa kipindi cha miaka sita. Kwa hiyo kuna utofauti wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na nilitaarifu tu Bunge lako Tukufu kwamba, Taasisi

yetu ya Elimu Tanzania *(TET)* na ile ya Zanzibar *(ZIE)* zinafanya kazi kwa karibu sana kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mitaala unakwenda sawasawa lakini na majadiliano ya karibu kuhakikisha kwamba changamoto zote zinazotokea kwenye utekelezaji wa mitaala zinapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pasipokuwa na shaka kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanza sasa kufanya mapitio ya Sera ile ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2016 na wataangalia sasa namna gani tunaweza kuhusianisha miaka hii ya Elimu ya Msingi kuhakikisha kwamba tunakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba tuna mjadala mpana wa kitaifa kuhakikisha kwamba mwenendo au mfumo wa elimu yetu uwe vipi.

Kwa hiyo, katika majadiliano haya tunaamini changamoto hizi zote anazozungumza Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge humu ndani zinaenda kupata ufumbuzi ikiwemo na hili la kuwa na mtaala mmoja kuanzia Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaelekea maji, swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Kalenga, uliza swali lako Mheshimiwa.

Na. 62

**Mradi wa Jumuiya ya Watumiaji Maji wa Magubike**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kiasi cha shilingi milioni 200 zilizoahidiwa na Waziri wa Maji Mwaka 2017 alipotembelea mradi wa Jumuiya ya Watumiaji Maji wa Magubike Kata ya Nzihi uliokarabatiwa na *WARID* kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.3?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la maji, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Kijiji cha Magubike upo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Mradi huo unahudumia vijiji sita vya Kata ya Nzihi ambavyo ni Nzihi, Kipera, Kidamali, Nyamihuu, Magubike na Ilalasimba. Kwa lengo la kuboresha huduma ya maji katika vijiji hivyo na kufikisha huduma ya maji katika vitongoji vingine ambavyo havina huduma ya maji, mwaka 2017 Waziri wa Maji aliahidi kutuma shilingi milioni 200 kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa Magubike.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi hiyo, Serikali mwezi Juni na Agosti, 2021 imetuma jumla ya shilingi milioni 180 ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita tisini elfu katika kijiji cha Nzihi, ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 11.25 kwa ajili ya jamii kuingiza maji majumbani. Ujenzi huo unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2021 na kukamilika ifikapo mwezi Januari 2022. Kukamilika kwa kazi hizo kutaboresha huduma ya maji katika vijiji husika pamoja na vitongoji vya Mji mwema B, Mbega na Kayungwa ambavyo havina huduma ya uhakika ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, swali la nyongeza tafadhali,

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru pamoja na majibu mazuri yanayoonesha Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ipo kazini, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kule Magunga kwenda Lumuli kulikuwa na mradi ambao uliasisiwa na Dkt. William Mgimwa, lakini hapo katikati ulikuwa umelala. Sasa tunaishukuru Serikali

imepeleka kiasi kama cha milioni 200 kutengeneza tenki kwa kutumia *force account...*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga sikuoni!

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, hunioni?

**SPIKA:** Sasa nakuona. *(Kicheko)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kule Magunga ukitoka Magunga kwenda Lumuli kuna mradi ambao ulihasisiwa na Marehemu Dkt. William Mgimwa zaidi ya miaka saba iliyopita bahati mbaya haukutekelezwa, lakini sasa tunaishukuru Serikali imepeleka kiasi cha milioni kama 200 hivi kuanza kwa kutengeneza tenki kwa kutumia *force account*, lakini ninaona kwamba kasi yake ni ndogo.

Je, Wizara ina mpango gani hata kwa kutumia Wakandarasi ili maji yale yafike Kata ya Lumuli ambapo wananchi wake wamesubiria kwa muda mrefu sana.*(Makofi)*

Swali la pili, kumekuwa na mradi ambao pia ulianzishwa na aliyekuwa Mbunge na Katibu wa Bunge hili George Francis Mlawa wa Nyamlenge. Mradi huu ulikuwa wa maji tiririka ambao ungezifikia Kata kama tano, ukianzia Lyamgugo, Luhota, Mgama, Bagulilwa mpaka Ifunda, lakini sasa mmebadilisha *scope* mnachimba visima, wasiwasi wangu ni kwamba ikitokea tetemeko la ardhi na kule tupo kwenye bonde la ufa, visima vile mkondo huwa unahama maji yanakosekana.

Je, Serikali sasa ina mpango gani kupeleka pesa za kutosha ili turudi kwenye *scope* ya zamani na maji yapatikane katika Kata hizo tano ambazo nimezitaja?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhali.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiswaga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru Mheshimiwa Kiswaga kwa kuishukuru Serikali ya Mama Samia, tayari Magunga kazi zinaendela pale tumeanza na hii milioni 200 lakini fedha tutaendelea kuleta kwenye migao inayofuata, lengo ni kuona wananchi wote wa eneo lile wanaendelea kupata maji ya uhakika ya kiwa safi na salama bombani.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Lumuli hapa kipo kwenye mpango wa fedha za mwaka 2021/2022 na mradi huu kadri ambavyo tumeweza kufanya mashirikiano na Mheshimiwa Mbunge tutautekeleza kwa kupitia Mkandarasi lengo iweze kufanyika kwa haraka na wananchi wa Lumuli nao waweze kunufaika na fedha hizi ambazo Mheshimiwa Rais ameendelea kutupatia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, eneo la Nyamulenge pia lipo kwenye mpango wetu wa muda mrefu. Kwa sasa hivi tumechimba visima virefu ambavyo vinatumia *pump* za umeme kwa sababu ya kuona kwamba kwa muda huu wananchi waweze kuendelea kupata huduma ya maji. Lakini katika mipango ya muda mrefu kama ambavyo tumeendelea kuwasiliana mara kwa mara na tulishaweza kushauriana kwa muda mrefu katika mpango wa muda mrefu chanzo hiki cha Nyamlenge tutakuja kukitumia kwa mradi wa maji ya uhakika maji ya mserereko ambayo eneo lile litapata maji ya kutosha na vijiji vyote vinavyopitiwa na mradi huu vitaweza kunifaika.

**SPIKA:** Ashante sana. Mheshimiwa Neema nilikuona.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Mkoa wa Njombe Wilaya ya Wanging'ombe kuna mradi wa maji wa Igando - Kijombe wenye thamani ya bilioni 12. Lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza ni bilioni mbili tu ambazo zimekwenda kwenye mradi ule na mkandarasi yuko *site* lakini amesimamisha mradi hule hauendelei kwa sababu Serikali haijapeleka pesa.

Je, lini Serikali itapeleka hizo bilioni 10 ili mradi ule uweze kukamilika na Wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Spika, hili suala tumeshalifanyia kazi kama Wizara na kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa nae Mheshimiwa Neema pamoja na Mheshimiwa Dkt. Dugange, tumeweza kufatilia na fedha tutaleta mgao ujao tutaendelea kutoa fedha kidogo kidogo, tutaleta bilioni Moja ili kazi ziendelee na mgao unaofuata pia tutaendelea kuleta fedha kadri tunavyopata.

**SPIKA:** Tuendelee Waheshimiwa na Katiba na Sheria, swali linaulizwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar Mbunge wa Nyang'hwale.

Na. 63

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya ya Nyang'hwale?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, tafadhali, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Nyang'hwale ni moja ya miradi itakayojengwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Zabuni ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo imekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Septemba mara baada ya kusainiwa kwa mkataba wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza programu iliyojiwekea ya kujenga na kukarabati majengo yote katika ngazi mbalimbali za Mahakama ili kusogeza huduma karibu na wananchi na kuboresha mazingira ya kazi ili kufikia lengo la kuwa na Mahakama za Wilaya katika Wilaya zote hapa nchini ifikapo 2025. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Kwa kuwa, Wilaya ya Nyang'hwale ina upungufu mkubwa sana wa Mahakama za Mwanzo, napenda kuiomba Serikali ianzishe *Mobile Court* katika Kata za Busolwa, Nyang'hwale, Kaboha na Shabaka; kwa kuwa Wilaya ya Nyang'hwale ina upungufu wa watumishi kama vile Mahakimu na Makarani.

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Mahakama hizo?

Swali la pili; je, Serikali ipo tayari kutuongezea Mahakimu pamoja na Watumishi kama vile Makarani?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nassor Amar Hussein, Mbunge wa Nyang'wale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza hili la *mobile court* tumelipokea na tutalifanyia kazi ili kuona uwezekano wa kata hizo ambazo hazijapata majengo ziweze kufikiwa na huduma hii.

Mheshimwia Spika, lakini vile vile, kuhusu watumishi tunaendelea kutegemeana na nguvu ya Serikali katika kupata uwezo wa kuajiri. Tunachoweza kuahidi tu ni kwamba tutakapopata nafasi ya kuajiri basi tutaangalia na suala la kupeleka watumishi katika maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anayaeleza. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, uliza swali lako.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wilaya ya Rungwe Mahakama yake ya Wilaya ni jengo la siku nyingi sana. Ni lini Serikali itatusaidia kujenga jengo jipya ambalo litakidhi vigezo vya kuweka wafanyakazi na kuwa na nafasi nzuri ili waweze kufanyakazi kwa weledi na kwa ufasaha zaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda

ambalo anataka kujua lini Serikali itajenga Mahakama katika Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, Mahakama iko kwenye mpango ambao ni wa kipindi hiki tulichonacho cha mwaka wa fedha kuanzia mwaka 2021 mpaka 2025. Katika kipindi hicho tutahakikisha maeneo yote ambayo hayana Mahakama za Wilaya majengo mapya yanaenda kujengwa kwenye maeneo yote ambayo hayana Mahakama za Wilaya.

Kwa sasa hivi kwenye eneo hilo la ujenzi ni matarajio yangu kwamba ifikapo mwaka 2025 eneo hili la Mahakama tutakuwa tumeshamaliza kabisa shughuli za ujenzi. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwamba, tunakwenda kukujengea hii Mahakama katika kipindi cha awamu hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado tuko Katiba na Sheria. Swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

Na. 64

**Mahakama Kugharamia Chakula cha Mahabusu**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Mahakama isipewe jukumu la kugharamia chakula cha mahabusu ambao wapo gerezani kutokana na ucheleweshaji wa kesi kupatiwa hukumu?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge liangalieni swali hili. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Magereza wapo kwenye wajibu wao wa kisheria wa kutoa huduma ya chakula kwa mahabusu. Hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Magereza Sura ya 58 (105) ambacho kinatoa mamlaka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutunga Kanuni *(The Prison Management Regulations)* ambapo Kifungu cha 23 cha kanuni iliyotokana na sheria hiyo kimemuelekeza Mkuu wa Magereza kusimamia chakula kwa wafungwa na mahabusu wanapokuwa gerezani kama sehemu ya wajibu wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mahakama haijawahi kuchelewesha utoaji wa maamuzi ya mashauri mbalimbali bila uwepo wa sababu muhimu zinazochangia kucheleweshwa kwa kesi husika. Wote tunafahamu kuwa vipo vyombo mbalimbali vinavyohusika katika suala la kesi. Vyombo hivi ni kama Polisi, Magereza, TAKUKURU, Ofisi za Mashtaka, Ofisi ya Mkemia Mkuu na kadhalika, kabla ya kuifikia Mahakama.

Mheshimiwa Spika, hivyo katika sura ya kawaida huonekana kuwa Mahakama ndizo zinazochelewesha utoaji wa hukumu, lakini ukweli ni kwamba kesi huchakatwa na vyombo nilivyovitaja; na wakati mwingine mchakato huchukua muda mrefu kabla ya kutoa nafasi kwa Mahakama kutoa maamuzi. Hata hivyo ninatoa wito kwa vyombo husika kuharakisha michakato inayopita kwenye vyombo vyao ili kufanya Mahakama kutoa hukumu kwa wakati na hivyo kufanya wananchi kupata haki zao kwa wakati. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Hapa ningependa kuikumbusha Serikali, kwamba si mara moja, mara mbili, mara tatu; na hata hivi karibuni tarehe 25 Agosti tulimsikia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akilisemea eneo hili la ucheleweshaji wa kesi kufikia hukumu na idadi

kubwa ya mahabusu. Vilevile, tulishamsikia Jaji Mkuu wa Mahakama zetu hapa nchini akilisemea pia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa idadi ya mahabusu ni 17,000 ukilinganisha na idadi ya wafungwa ambayo ni 14,000; na wakati huo huo Serikali haitoi bajeti ya aina yoyote kwa ajili ya chakula; kwa sababu Magereza imepewa maelekezo kwamba ijitegemee kwenye chakula, sasa wale wafungwa 14,000 wanazalisha chakula kwa ajili ya kujilisha wao wenyewe na pia kulisha wale mahabusu 17,000. Je, Serikali haioni ipo haja ya kupitia upya Sheria ile ili itafute namna ya kuwawezesha hawa mahabusu angalau wazalishe chakula chao wenyewe wanachokula?

Mheshimiwa Spika, na swali langu la pili, kwa kuwa majibu ya Serikali wamesema kwamba viko vyombo mbalimbali ambavyo vinahusika kwenye kutoa hukumu hizi za kesi. Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuweka ukomo wa muda ambao utatumika kuanzia upelelezi mpaka kutolewa kwa hukumu kwa kulingana na uzito wa kesi zenyewe? Kwa sababu, ukweli ni kwamba, tuchukulie mfano mtu amebaka halafu kesi yake inaendelea kwa miaka 10...

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema inatakiwa swali. *(Kicheko)*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, sawa. Kwa hiyo swali langu ni kwamba, je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kupitia upya mfumo mzima wa Mahakama na kuweka ukomo wa muda wa upelelezi mpaka kutoa hukumu? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Lugangira kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hili la kupitisha sheria ili mahabusu waanze kufanya kazi wakati wakisubiri kesi zao kimsingi ni jambo ambalo tutakuwa tunavunja vile vile haki za binadamu. Kwa sababu wakati mtu anasubiri upelelezi wake wa kesi hajahukumiwa kuwa mfungwa, ukianza kumfanyisha kazi maana yake umemhukumu kabla ya wakati wake. Kwa hiyo, mahabusu huwa wanafanya kazi ndogo ndogo tu za usafi wa mazingira waliyopo, lakini si kuwafanyisha kazi kama wafungwa. Kwa sababu, mfungwa kifungo chake kinamruhusu sasa kufanyishwa kazi kwa ajili ya kurekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili suala la ukomo wa upelelezi, tunao ukomo wa upelelezi kutegemeana na mazingira ya kesi yenyewe. Kwa mfano, kesi nyingine zimepewa siku 60, kesi nyingine zina miezi sita, lakini kesi nyingine kulingana na mazingira yake zinaweza zikaenda muda mrefu; kwa mfano kesi za mauaji. Kwa hiyo hili linatekelezwa Kisheria.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa kama nilivyotoa maelezo yangu kwenye jibu la msingi, kuvitaka vile vyombo vinavyohusika na michakato kuharakisha michakato. Hiyo itasaidia sana kupunguza baadhi ya kesi ambazo kimsingi zinapelekwa pale lakini zinakuwa hazina mashiko ya kuendelea kuwa Mahakamani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, muuliza swali hana uzoefu sana na mambo haya, sasa ngoja twende kwa wazoefu. Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Esther Matiko. Tunaanza na Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali alisema kwamba, kesi zinachelewa kwa sababu kuna vyombo mbalimbali vinachakata. Lakini labda nikuulize Mheshimiwa Waziri, hivi kuanzia mwaka 0 mpaka miaka 7, vyombo kuendelea kuchakata wakati watu wako magereza, unadhani ni sawa? na kama si sawa, kwanini sasa, badala ya kutoa maagizo hapa Bungeni usiwe ni wakati muafaka kwa Serikali kufanya

kazi ya ziada kwenda kuchunguza kinagaubaga ili kuja na majibu ambayo yatasaidia wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Geofrey Mizengo Pinda, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, muda wa kukaa mahabusu utategemea mwenendo wa upelelezi, na hivyo ni halali kabisa wakati mtu anapelelezwa, ambaye atakuwa yuko nje ya vigezo vya dhamana kuendelea kuwa chini ya Magereza. Kwa hiyo muda unaangaliwa na uzito.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusu uchunguzi, kwamba tuunde timu ambayo itasaidia kuangalia kwa ukaribu na kwenda kufanya utafiti wa kina badala ya kutoa maagizo Bungeni; hapa nilikuwa natoa kama msisitizo tu lakini ukweli Serikali tulishaanza hiyo kazi na ukweli kwa kipindi hiki cha kuanzia Januari mpaka sasa naamini wazi watu wote mnaona kasi ya kuondoa mahabusu wasiokuwa na kesi zenye mashiko imeongezeka sana na mahabusu zimeanza kupumua. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, nilishakutaja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ucheleweshaji wa kesi kwa kiasi kikubwa unatokana na upelelezi kutokamilika kwa muda muafaka, na kwa kuwa kuna kesi ambazo, kwa mfano, kuna kesi moja mahabusu amekaa zaidi ya miezi 8, *house girl* kaiba sijui vitenge viwili kwa mwajiri wake, kesi haikamiliki. Swali langu ninataka kujua; kwa kuwa kesi zinakuwa hazikamiliki, watu wanakaa miaka 8, 10 mpaka 12. Ni kwa nini sasa upelelezi usifanyike ukikamilika sasa, ikifikia hatua ya usikilizaji ndipo watuhumiwa waweze kupelekwa mahakamani, ambapo ndipo itachukua muda watu wasikae magerezani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Simbachawene, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa si kila kesi mtuhumiwa anatakiwa kukaa mahabusu, ni baadhi ya kesi ambazo zimetajwa kwa mujibu wa Sheria, kwamba kwa makosa ya aina hii mtuhumiwa hapaswi kuachwa huru. Anatakiwa azuiwe kwa sababu kwanza yeye mwenyewe anaweza akahatarisha maisha yake kutokana na *nature* ya kosa alilokosa, lakini pili akiwa nje anaweza akaharibu upelelezi, kwa maana ya kesi husika kulingana na hukumu na ukubwa wa kesi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hawa ambao wanatuhumiwa kubaki kwa kesi ya vitenge kama anavyosema, hii ni kesi tofauti na pengine ni kesi moja kwa nyingine. Nitoe rai na niseme tu kwamba, kwa yale makosa ambayo, na wewe unafahamu, yanahitaji kabisa dhamana na dhamana ni haki ya mshitakiwa; lakini kwa makusudi tu inazuiwa kutolewa dhamana na sheria inasema kosa hilo linadhaminika; kwamba hiki kitendo hakikubaliki na ni lazima tufuate sheria, sote tuondoe mahabusu kuwa wengi kwa kufanya hivyo. Kwa sababu, kwa kufanya hivyo kutatusaidia sana kupunguza idadi ya mahabusu wengi tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu, Serikali hata mara moja, lakini pia hata Idara ya Upelelezi ndani ya Jeshi la Polisi haiwezi hata mara moja ikarefusha upelelezi kwa kesi ambayo inahitaji kumalizwa upelelezi wake. Bali kama kuna jambo limetokea mimi niletewe tushughulikie. Kama kuna kesi ya khanga, kesi ya vitenge, kesi ya bakuli amefanya *house girl* akakaa miezi minane, ni jambo maalum la kushughulikiwa na nitaomba Mheshimiwa Mbunge tuonane naye ili aweze kunipa taarifa zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge na sisi kupitia Kamati zetu mbalimbali tuangalie na sisi mchango wetu katika jambo hili. Unakuta kila tunapotunga sheria si kuna adhabu kule mbele; unafunga watu miaka sijui 20, 15, ngapi! Dunia ya leo ilivyo *faster* ukimfunga mtu mwaka yaani kama ni mtu wa kurekebika amerekebika sana huyo.

Ukimfunga miaka mitatu siku anatoka yaani dunia anaikuta imebadilika kiasi kwamba; yaani si kama miaka ile ya sitini na ngapi kule tulikuwa tunafunga watu. Sasa hivi tuangalie na sisi tunapotunga sheria zetu; kwa sababu na sisi ni sehemu ya sababu ya mlundikano wa wafungwa kwa namna moja au nyingine kwa namna ya ambavyo tunatunga aina ya adhabu zetu. Kwa hiyo na sisi tubadilike kidogo, tuangalie. *(Makofi)*

Swali la mwisho kwa siku ya leo Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Ali Juma Mohamed. Mheshimiwa Ali.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba jibu langu namba 65 liweze kupata majibu ya serikali.

**SPIKA:** Swali lako! siyo jibu lako.

Na. 65

**Serikali Kusimamia Mikataba ya Vijana Wanaofanya Kazi Nje ya Nchi**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia Balozi zetu ina mkakati gani wa kusimamia mikataba ya vijana wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi?

**SPIKA:** Ahsante, majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha Watanzania wanaopata fursa za ajira nje ya mipaka ya Tanzania wanafanya kazi katika mazingira mazuri na yanayolinda staha na utu wao. Katika kufanikisha azma hiyo Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kutoa vibali vya ajira nje kupitia mamlaka zinazoshughulikia masuala ya ajira, ikiwemo Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TAESA)* na Kamisheni ya Kazi Zanzibar kwa kushirikiana na Balozi za Tanzania nje.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo pamoja na mambo mengine unaelekeza kila mfanyakazi kuwa na wakala rasmi wa ajira, ambaye anatambuliwa na mamlaka tajwa ambao ndio waandaaji wa mikataba ya ajira nje inayopaswa kukidhi Sheria za Ajira za Tanzania na nchi anayokwenda kufanya kazi. Aidha, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Serikali mikataba hiyo pia inapaswa kuandaliwa kwa lugha inayoeleweka na vijana hao, ikiwemo Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuweka utaratibu huo bado kumekuwa na changamoto zinazotokana na baadhi ya vijana wanaopata ajira nje kutozingatia utaratibu uliopo. Pia, baadhi ya vijana hao hawajitambulishi kwenye Ofisi za Balozi za Tanzania pindi wanapofika kwenye ajira zao Ughaibuni. Kutokana na hali hiyo Serikali kupitia Balozi zake imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) kutambua Kampuni za Uwakala wa Ajira za Nje na kuzitaka ziwe na uhusiano wa kimkataba na Kampuni za Uwakala za Tanzania.

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa vijana wanaopata ajira nje kutoa taarifa zao na kuwasilisha nakala za mikataba yao ya ajira Balozini ili ziweze kuhakikiwa.

(iii) Serikali imeanza mchakato wa kuingia mikataba ya ajira na baadhi ya nchi ili kurasimisha upatikanaji wa ajira katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Watanzania ambao wana nia ya kufanya kazi nje ya mipaka ya Tanzania, kufuata utaratibu uliowekwa na mamlaka husika. Kwa kuwa pamoja na mambo mengine inawapa kinga na kuepuka mazingira mabaya ya kazi ambayo hayatarajiwi na pia kurahisisha kupata msaada pale unapohitajika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali, swali la nyongeza.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na swali moja tu la nyongeza.

Serikali ina mpango gani wa kutafuta fursa mbalimbali za ajira ambazo ziko katika nchi mbalimbali duniani, kwa ajili ya Watanzania hususan nchi ya *Qatar* ambayo mwakani ni wenyeji wa Kombe la Dunia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje, Mheshimiwa Balozi Mbarouk.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuchangamkia fursa kwa ajili ya Watanzania kwenda kufanya kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kukufahamisha kuwa Serikali imeanza mazungumzo na nchi mbalimbali ambazo zina fursa ya ajira hizo, hasa zikiwemo nchi za Ghuba, ili kuwa na utaratibu maalum wa kutoa *quarter* maalum kwa ajili ya Tanzania. Ninapenda kutoa taarifa pia kwamba tayari

Tanzania imesaini mkataba na nchi ya *Qatar* kwa ajili ya kuwa na *quarter* maalum ya watanzania kwenda kufanya kazi huko, hasa katika kipindi hiki ambako tunaelekea kwenye mashindano ya *World Cup* ambayo yanaanza Novemba mwakani 2022. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunapaswa kuendelea. Tulitoa lawama kidogo kwa Kamati yetu ya Bajeti kuhusiana na ile asilimia mbili (2%) ya *withholding tax.* Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, ameniandikia hapa kunikumbusha tu, anasema, naomba kukuarifu kuwa suala la *withholding tax* asilimia mbili (2%) kwenye mazao ya kilimo Kamati yetu ya Bajeti iliiliona wakati ule na Kamati ililipinga sana. Wakati wa majumuisho ya *Finance Bill* likawemo lakini pamoja na hayo hata kwenye Taarifa ya Kamati yetu tuliyowasilisha katika Bunge lako Tukufu tulitamka wazi msimamo wetu wa Kamati kupinga jambo hilo, inaelekea tu utekelezaji umekuwa tofauti.

Tunajifunza nini hapa? Ukiona kitu Kamati imekikataa, Waheshimiwa Mawaziri ukiking'ang'ania, sawa unang'ang'ania lakini mwisho wa siku ni *disaster* tu, sasa ndiyo mambo ya namna hii. Mara nyingi mwisho wa siku tunakubaliana na Serikali lakini sasa lazima kuangalia. Hivi vitu ni tatizo kubwa, tukumbuke sisi ni matokeo ya kura, unapopeleka kodi kwa wakulima kundi kubwa namna hiyo unajitakia matatizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali ikalitazame jambo hili na ichukue maoni ya Wizara ya Kilimo ambayo wameshapeleka kule. Twende taratibu na haya mambo na hasa kama Kamati imeshashauri. Pia wakati mwingine Kamati muwe mnatuambia mapema, kwa kawaida Bunge lolote linasimama na Kamati yake, nafikiri hata Bunge hili litakuwa hivyo. Mkiona jambo Kamati imesimamia kabisa basi tunapofika wakati wa kupiga kura tunasimama na Kamati katika mambo haya ya msingi, Waziri anabaki peke yake. Ndiyo maana tunashauriana sana huko, si nia yetu kufika

hapo lakini nia yetu ni kwamba tuzungumze kwenye Kamati mpaka tuelewane. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati anaponiandikia kwamba jambo hili lipo tayari maana yake mmeelewana lakini kama kuna eneo ambalo mna-*feel* kabisa kama Kamati ni *strong* basi mnatuambia mapema na litavukaje, mbona haliwezi kuvuka. *(Makofi)*

Wageni waliopo katika Jukwaa la Spika ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ni Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Christopher Kadio; Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Ramadhani Kailima; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna John Masunga; na Naibu Kamishna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Nassa Rwahila. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine nitawatambulisha baadaye nikishapata maelezo yao. Naona karatasi yangu hapa haina majina yao.

Waheshimiwa Wabunge, juzi tulikuwa na siku maalum kabisa ya michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya NMB, Mheshimiwa Abbas Tarimba hapa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* ameniletea matokeo ya kazi ya juzi kama ambavyo nilikuwa nimewaonya NMB kwamba Bunge siyo masihara, naomba nitangaze matokeo kama ifuatavyo. *(Kicheko)*

Riadha mita 100 wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Rose Tweve. Mita 400 wanawake mshindi alikuwa Teddy George wa NMB. Riadha mita 100 na 400 wanaume mshindi alikuwa Sollo Mlozi wa NMB. Mbio za viongozi mita 100 wanawake mshindi ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. *(Makofi)*

Kuvuta Kamba wanaume na wanawake mshindi wa *Bunge Sport Club*, nyota wa michezo kwa upande wa wanaume alikuwa Mheshimiwa Agustino Vuma. Kuvuta Kamba kwa upande wa wanawake nyota alikuwa Mheshiwa

Sophia Mwakagenda. Niliwaonya *NMB* kuhusu kuvuta kamba mchezo huu hawatuwezi kabisa kwa sababu haya mambo yanaendana na lishe na kantini ya Bunge ipo vizuri. *(Makofi/ Kicheko)*

Mpira wa pete *(netball), Bunge Sports Club* 25 - NMB tatu. Nyota wa mpira wa pete kwa upande wa Wabunge alikuwa Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk. *(Makofi)*

Mpira wa wavu *(volleyball)* upande wa wanaume *Bunge Sports Club* ilipata seti 2 na *NMB* hakupata kitu. Nyota wa mchezo wa mpira wa *volleyball* kwa upande wa wanaume alikuwa Mheshimiwa Antipas Mgungusi, hongera sana. Mpira wa wavu *volleyball* kwa upande wa wanawake *Bunge Sports Club* seti 2 – NMB hawakupata kitu. Nyota wa mchezo huo wa *volleyball* kwa upande wa Wabunge alikuwa Mheshimiwa Jesca Kishoa. *(Makofi)*

Mpira wa kikapu (*basketball) Bunge Sports Club* walipata magoli 70, *NMB* 50. Nyota wa mchezo wa *basketball* alikuwa Mheshimiwa Dennis Londo. *(Makofi)*

Mchezo wa kufukuza kuku, mshindi alikuwa Mheshimiwa Saada Monsour Hussein. *(Makofi)*

Mchezo wa mpira wa miguu washindi walikuwa ni *Bunge Sports Club* kwa kufunga *penalty* 4 dhidi ya *NMB penalty* tatu. Mchezaji bora wa siku hiyo alikuwa Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki. *(Makofi)*

Kwa niaba yenu, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana *NMB* kwa jinsi ambavyo kwa kweli wameifanya siku yetu ya Jumamosi kuwa nzuri sana. Tulizungumza nao wamekubali kwamba Bunge lijalo watakuja kivingine. Kwa hiyo, Waheshimiwa muendelee na mazoezi katika Mkutano ujao wa Bunge tutakuwa tena na siku nyingine sisi pamoja na *NMB*. *Theme* ya safari hii walisaidia upande wa elimu kwa kutoa *ream* za karatasi pamoja na pedi za watoto wa kike. *Theme* ya safari ijayo itahusiana na masuala ya mazingira na upandaji miti. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendments) Bill, 2021)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA*:*** Kusomwa Mara ya Pili, sasa moja kwa moja nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aweze kutupitisha kwenye hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Waziri uwasilishe hoja yako, tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2020, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendments) Bill, 2021),* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia neema zake na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Nne wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi wetu wote wakuu kwa namna wanavyoongoza nchi yetu kwa uzalendo, ujasiri na kuzingatia

malengo na maono yao na hivyo kuliletea Taifa letu maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti kwa namna ambavyo mnaliongoza Bunge letu katika mafanikio makubwa ya kusimamia nchi yetu lakini pia kuisimamia Serikali na kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Adelardus Kilangi, pamoja na ofisi yake yote na hasa zaidi Mwandishi Mkuu wa Sheria Ndugu Onorius Njole kwa namna alivyoshirikiana na Wizara yetu katika kuandaa Muswada huu. Nimshukuru pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Mussa Zungu pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa namna ambavyo tunafanya nao kazi kirafiki lakini pia kwa uangalifu mkubwa na kwa mafanikio makubwa na hata kufikia kukamilisha Muswada huu. Karibu maeneo yote tumeelewana vizuri sana, yale waliyotuambia tuondoe tumeondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa masikitiko makubwa, nitoe pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan lakini kwako wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kutokana na kifo kilichompata Ndugu yetu aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nichukue nafasi hii pia kuwapa pole wananchi wote waliofikwa na majanga mbalimbali ya moto hapa nchini na kupoteza mali zao na wengine kupoteza ndugu zao. Tunawapa pole tukiamini kwamba mabadiliko ya sheria hizi yataleta ufanisi na kuhakikisha kwamba majanga yanapungua kama siyo kuondoka kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Mussa Zungu kama nilivyosema katika maelezo yangu ya awali pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi yetu kuwa nzuri sana kwa kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu na kama nilivyosema katika maeneo yote tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya sheria hiyo na sheria nyingine. Madhumuni ya marekebisho ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura ya 427 ni kuziba ombwe na kuzikabili changamoto zinazokabili katika usimamizi na utekelezaji wa sheria katika kulinda na kuokoa maisha ya watu na mali zao wakati wa majanga. Marekebisho haya pia yanakusudia kuhakikisha shughuli za zimamoto na uokoaji zinafanyika kwa ufanisi nchini ili kuendelea kuwavutia wawekezaji kwa kuwahakikishia usalama wa maisha na mali zao; kuweka viwango vya madaraja ya huduma za zimamoto na uokoaji zinazotolewa na kampuni binafsi; pia yanalenga kuhuisha viwango vya adhabu na faini zinazotozwa na mahakama.

Mheshimiwa Spika, lakini pia marekebisho haya yanaweka masharti kwenye majengo yenye urefu wa mita 12 au zaidi ambayo ni sawa na ghorofa tatu ili kuhakikisha wanafunga mifumo ya kung'amua na kuzimia moto ili kupunguza majanga yanayoweza kuepukika. Lengo la marekebisho haya kwa ujumla ni kuleta tija katika usimamizi wa sheria hii ili kulinda maisha ya watu na mali zao na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya neno 'mzimamoto' lililotumika katika sheria. Madhumuni ya marekebisho haya ni kutofautisha kati ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Mzimamoto mwingine kwa kuwa Askari wote wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni Wazimamoto lakini Wazimamoto wote siyo Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza Marekebisho ya kifungu cha 5(2) cha Sheria kwa kufuta aya ya (f) na badala yake kuweka aya mpya kwa lengo la kutoa jukumu la kuanzisha na kutunza kanzidata ya huduma ya zimamoto na uokoaji zinazotolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kampuni binafsi saidizi zinazotoa huduma za zimamoto na uokoaji na mawakala wa usambazaji na uuzaji wa vifaa vya zimamoto ili kurahisisha upatikanaji takwimu za matukio na kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kujipanga kimkakati katika kuboresha huduma zake.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho ya kuongeza kifungu kipya cha 11A ili kuwapa Askali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haki ya kutumia silaha wakati wa utekelezaji wa majukumu, wajibu na mamlaka yao yanayoaishishwa chini ya sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha usalama wa miundombinu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Maafisa, Askari na pia silaha hizo kutumika katika mafunzo.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho kifungu cha 13 kuhusiana na visima vya maji ya kuzima moto na usambazaji wa maji yaani *fire hydrants* ili kuhakikisha kuwa maji yanapatikana bila kizuizi katika maeneo yaliyoainishwa. Marekebisho yanayopendekezwa ya kifungu cha 13(3) yanakusudia kuweka ukomo wa adhabu kwa watakaoharibu miundombinu ya maji baada ya marekebisho haya kwa kuweka faini iliyopungua shilingi laki mbili na na isiyozidi shilingi laki tatu ili kuhakikisha wananchi wanatunza mbiundombinu ya kupambana na majanga ya moto. Marekebisho yayonakusudiwa katika kifungu cha 13(5) yanalenga kutoa adhabu kwa wakosaji wanaofanya makosa

kwa kujirudia. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa yaliyoainishwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho kifungu cha 14(3) kwa lengo la kutenganisha mamlaka ya ajira ya Maafisa wa Zimamoto na Uokoaji wa cheo cha Mkaguzi Msaidizi hadi Kamishna Msaidizi kusimamiwa na Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza na wakati mamlaka ya ajira ya Askari wa Zimamoto na Uokoaji wa cheo chini ya Mkaguzi Msaidizi kusimamiwa na Kamishna Jenerali. Vilevile marekebisho yanapendekeza katika kifungu cha 19 kumpa uwezo Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuzingatia amri na maelekezo ya Waziri kutengeneza amri ya usimamizi wa jumla wa Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha 22(1) kwa kumtaka mmiliki au mtumiaji wa jengo kuwajibika kufunga mfumo wa vifaa vya moto kwenye jengo lenye urefu wa mita 12 na zaidi juu ya usawa wa ardhi sawa na ghorofa tatu. Marekebisho yanayopendekezwa pia katika kifungu kidogo (2) kumtaka mmiliki au mtumiaji wa jengo lenye urefu mita 12 juu ya usawa wa ardhi kuwasilisha Jeshini michoro ya ujenzi wa jengo kabla ya utolewaji wa kibali cha ujenzi utakaofanywa baada ya kupita kwa marekebisho haya. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuongeza mawanda ya usalama wa moto kwenye majengo.

Mheshimiwa Spika, Muswada pia unapendekeza marekebisho katika sheria kwa kuongeza vifungu vya 31A na 31B kwa kuweka masharti, adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayakuwekewa adhabu na ufifilishaji wa makosa mtawalia. Malengo ya marekebisho haya ni kuwezesha usuluhishi na kupunguza mlolongo mrefu wa mashauri mahakamani pale inapobidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 32 ili kuongeza wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kutengeneza kanuni

zikiwemo Kanuni kwa ajili Kampuni Binafsi Saidizi zinazotoa huduma ya zimamoto na uokoaji na Mawakala wa Uuzaji na Usambazaji wa Vifaa vya Kuzimamoto na Uokoaji. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuweka masharti ya kusimamia na kudhibiti huduma ya zimamoto na uokoaji zinazotolewa Tanzania Bara na watu binafsi na umma.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa marekebisho yatokanayo katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza, Sura ya 241 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 kama ifuatavyo: Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza, marekebisho yafanyike kwa ujumla kwa kufuta maneno Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza popote yatakapoonekana katika sheria na badala yake kuwekwe maneno, Jeshi la Polisi, Magereza, Jeshi la Zimamoto na Ukoaji na Uhamiaji.

Madhumuni ya marekebisho haya ni kujumuisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza.

Mheshimiwa Spika, kufuta maneno Maofisa wa Polisi, Uhamiaji na Magereza popote yatakapotokea katika Sheria na badala yake kuweka maneno Maafisa wa Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwajumuisha Maafisa wa Zimamoto na uokoaji katika orodha ya Maofisa wanaotambuliwa chini ya Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza.

Mheshimiwa Spika, kufuta maneno Inspekta Jenerali wa Polisi, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na Kamishna Mkuu wa Magereza popote yanapotokea katika sheria na badala yake kuweka maneno Inspeka Jenerali wa Polisi, Kamishna Mkuu wa Magereza, Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji. Madhumuni ya marekebisho haya ni kujumuisha Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji na kumpa mamlaka sawa na Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 4(2) ili kujumuisha Kamishna Jenerali, Kamishna wa Utawala na Fedha na Naibu Kamishna wa Sheria wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Tume. Lengo la marekebisho haya ni kujumuisha Wajumbe wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenye Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya jumla ya kurekebisha sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza na kulijumlisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambalo awali lilikuwa halihusiki na sheria hii katika utaratibu wa ajira, nidhamu na upandishwaji wa vyeo unaotumika na vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Kifungu cha 2 kinafanyiwa marekebisho katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuliongeza Jeshi la Zimamoto na uokoaji katika orodha ya majeshi. Lengo la marekebisho haya ni kulijumlisha Jeshi la Zimamoto katika orodha ambayo masharti ya Sheria ya Ajira na Mahusiano hayatatumika kwayo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru wewe na kama nilivyosema na Kamati ya NUU (Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama) kwa kutupa msaada mkubwa wa kutushauri na hadi sheria hii imefikia hatua hii na hata tumeweza kuwasilisha. Nichukue nafasi hii kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kuujadili na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

ISSN 0856 - 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 11*** ***25th August, 2021***

## *SPECIAL BILL SUPPLEMENT*

*To the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.10. Vol.101 dated 25th August, 2021*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

# THE FIRE AND RESCUE FORCE (AMENDMENT) ACT, 2021

## ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.

PART II
AMENDMENT OF THE FIRE AND RESCUE FORCE ACT,
(CAP. 427)

2. Construction.
3. Amendment of section 3.
4. Amendment of section 5.
5. Addition of section 11A.
6. Amendment of section 13.
7. Amendment of section 14.
8. Amendment of section 19.
9. Amendment of section 22.
10. Addition of sections 31A and 31B.
11. Addition of section 32.

PART III
CONSEQUENTIAL AMENDMENTS
*(a) The Police Force, Immigration and Prison Service Commission Act,*
*(Cap. 241)*

12. Construction.
13. General amendments.
14. Amendment of section 2.
15. Amendment of section 4.

*(b) The Employment and Labour Relations Act, (Cap. 366)*
16. Construction.
17. Amendment of section 2.

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
21st August, 2021

HUSSEIN A. KATTANGA
*Secretary to the Cabinet*

## A BILL
*for*

**An Act to amend the Fire and Rescue Force Act and to provide for other related matters.**

**ENACTED** by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

### PART I
### PRELIMINARY PROVISIONS

Short title

**1.** This Act may be cited as the Fire and Rescue Force (Amendment) Act, 2021.

### PART II
### AMENDMENT OF THE FIRE AND RESCUE FORCE ACT, (CAP. 427)

Construction
Cap. 427

**2.** This Part shall be read as one with the Fire and Rescue Force Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 3

**3.** The principal Act is amended by inserting in its appropriate alphabetical order the following definition:

Cap. 241

"“Commission” means the Commission established under section 4 of the Police Force, Tanzanian Immigration Services Department and Prisons Service Commission Act;

“voluntary firefighter” means any person who is ordered by the Minister pursuant to section 12 to fight fire and perform search and rescue service in accordance with the provisions of this Act;”.

Amendment of section 5

**4.** The principal Act is amended in section 5(2) by deleting paragraph (f) and substituting for it the following:

“(f) keep and maintain a database regarding fire and rescue service information;”.

Addition of section 11A

**5.** The principal Act is amended by adding immediately after section 11 the following:

“Entitlement to carry and use arms

**11A.** A fireman shall, when discharging his functions, duties or powers conferred to him under the Act, be entitled to carry and use arms.”.

Amendment of section 13

**6.** The principal Act is amended in section 13, by-

(a) deleting subsection (3) and substituting for it the following:

“(3) Any person who-

(a) uses a fire hydrant or other water supply or installation referred to in subsection (1), for any purpose other than that authorised by the Force; or

(b) covers up, encloses, tampers or conceals a fire hydrant or other water supply or installation,

commits an offence and shall be liable on summary conviction to a fine of not less than five hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings or to imprisonment for a term not exceeding one year or to both.”;

(b) adding immediately after subsection (4) the following:

"(5) Where a person convicted of an offence under this section is a subsequent offender for a similar offence, such person shall be liable on summary conviction-

(a) in the case of an offence under subsection (3), to a fine of not less than one million shillings but not exceeding five million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years; and

(b) in the case of an offence under subsection (4), to a fine of not less than three hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings or to imprisonment for a term of not less than three months but not exceeding one year.";

(c) renumbering subsection (5) as subsection (6).

Amendment of section 14

**7.** The principal Act is amended in section 14 by deleting subsection (3) and substituting for it the following:

"(3) The assistant commissioners and other officers of the rank of, or above assistant inspector of the Force shall be appointed by the Commission.

(4) The officers of the Force of the rank below assistant inspector shall be appointed by the Commissioner-General.".

Amendment of section 19

**8.** The principal Act is amended in section 19, by-

(a) deleting the word "Regulations" appearing in the marginal note and substituting for it the word "Orders";

(b) deleting subsection (1);

(c) designating the content of subsection (2) as section 19; and

(d) deleting the content of section 19 as designated and substituting for them the following:

"The Commissioner-General may, subject to this Act and directions of the Minister, make orders for the general governance of the Force in relation to-".

Amendment of section 22

**9.** The principal Act is amended in section 22-

(a) in the opening phrase of subsection (1) by deleting the words "more than twelve meters" and substituting for them the words "twelve meters and above,";

(b) in subsection (1), by deleting the word "or" appearing at the end of paragraph (b);

(c) by adding immediately after paragraph (b) as amended the following:

"(c) automatic fire sprinklers; or";

(d) by renaming paragraph (c) as paragraph (d);

(e) by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) The owner or operator of any building shall provide a building plan to the Force for inspection and fire safety advice prior to issuance of building permit by the relevant authority."; and

(f) by deleting the words "subsections (1) and (2)" appearing in subsection (3) and substituting for them the words "subsection (1)".

Addition of sections 31A and 31B

**10.** The principal Act is amended by adding immediately after section 31 the following:

"General penalty

**31A**. A person who commits an offence under this Act for which no specific penalty is provided, shall upon conviction, be liable to a fine of not less than five hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings or to imprisonment for a term of six months or both.

Compounding of offences

**31B.**-(1) Notwithstanding the provisions of this Act relating to penalties, where a person admits in writing that he has committed an offence under this Act, the Commissioner General or any officer of the force authorised by him in writing may, subject to the regulations made under subsection (7), at any time prior to the

commencement of the proceedings by a court of competent jurisdiction, compound such offence and order such person to pay a sum of money not exceeding one half of the amount of the fine to which such person would otherwise have been liable to pay if he had been convicted of such offence.

(2) Where a person fails to comply with the compounding order issued under this section within the prescribed period, the Commissioner General or an officer of the force authorised by him may, in addition to the sum ordered, require the person to pay an interest at the rate prescribed in the regulations.

(3) Where a person fails to comply with subsection (2), the Commissioner General may enforce the compounding order and interest accrued thereof in the same manner as a decree of a court.

(4) The Commissioner General shall submit quarterly report of all compounded offences under this section to the Director of Public Prosecutions.

(5) Any moneys charged under this section shall be paid into the Consolidated Fund through the Government Electronic Payment System.

(6) Where an offence is compounded in accordance with subsection (1) and proceedings are brought against the offender for the same offence, it shall be a good defence for the offender to prove to the satisfaction of the court that the offence with which the offender is charged has been compounded under subsection (1).

(7) The sum to be charged for every compoundable offence, forms and manner of compounding of offences shall be as prescribed in the regulations made under this Act.”.

Amendment of section 32

**11.** The principal Act is amended in section 32, by-

(a) adding immediately after paragraph (g) the following:

(h) registration or deregistration of auxiliary fire units and fire dealers;

(i) suspension or cancelation of certificate of registration;

(j) operations of auxiliary fire units and fire dealers;

(k) procedures for appeal;

(l) procedure for submission to the Force the statistics from auxiliary fire units and fire dealers;"; and

(b) renaming paragraphs (h) and (i) as paragraphs (n) and (o).

## PART III
## CONSEQUENTIAL AMENDMENTS

### *(a) The Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prison Service Commission Act, (Cap. 241)*

Construction Cap. 241

**12.** This Part shall be read as one with the Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prison Service Commission Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

General amendments

**13.** The principal Act is amended generally by-

(a) deleting the words "the Police Force, Immigration and Prison Service" appearing in the long title and substituting for them the words "the Police Force, Prisons Service, Fire and Rescue Force and Immigration";

(b) deleting the words "the Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prisons Service" wherever they appear in the Act and substituting for them the words "the Police Force, Prisons Service, Fire and Rescue Force and Tanzania Immigration Services Department";

(c) deleting the words "the police, immigration and prisons officers" wherever they appear in the Act

and substituting for them the words "the police, prisons, fire and rescue and immigration officers"; and

(d) deleting the words "the police, immigration or prisons officer" wherever they appear in the Act and substituting for them the words "the police, prisons, fire and rescue or immigration officers"; and

(e) deleting the words "Inspector General of Police, Commissioner-General of Immigration and Principal Commissioner of Prisons" wherever they appear in the Act and substituting for them the words "Inspector General of Police, Principal Commissioner of Prisons, Commissioner-General of Fire and Rescue and Commissioner-General of Immigration".

Amendment of section 2

**14**. The principal Act is amended in section 2 by adding in the appropriate alphabetical order the following definition:

"fire and rescue officer" includes a fire officer and a fireman;".

Amendment of section 4

**15**. The principal Act is amended in section 4(2), by-

(a) inserting immediately after paragraph (e) the following-

"(f) Commissioner-General of Fire and Rescue Force;";

(b) inserting immediately after paragraph (n) the following-

"(o) Commissioner of Fire and Rescue Administration and Finance;";

(c) inserting immediately after paragraph (p) the following-

"(q) Deputy Commissioner of Fire and Rescue Legal;"; and

(d) renaming paragraphs (f) to (o) as paragraphs (g) to (r) respectively.

*(b) The Employment and Labour Relations Act, (Cap. 366)*

Construction Cap. 366

**16.** This Part shall be read as one with the

Employment and Labour Relations Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**17.** The principal Act is amended in section 2(1), by-

(a) deleting the word "or" appearing at the end of paragraph (iii);

(b) deleting a full stop appearing at the end of paragraph (iv) and substituting for it a semicolon and the word "or"; and

(c) adding immediately after paragraph (iv) the following:

"(v) the Fire and Rescue Force.".

## OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend the Fire and Rescue Force Act, Cap. 427 and to make consequential amendments to the Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prison Service Commission Act, Cap. 241 and the Employment and Labour Relations Act, Cap. 366.

The proposed amendments intend to address the shortcomings observed during the implementation of the law and to effect amendments to other laws to be in line with the proposed changes.

The Bill is divided into three Parts, whereby Part I deals with Preliminary Provisions.

Part II of the Bill proposes amendment to the Fire and Rescue Force Act, Cap 427, whereby section 3 is amended by adding the interpretation of the terms so as to provide for the intended meaning. Section 5is proposed to be amended with the view to improve record keeping of the services rendered by the Force through a database.

The amendment proposes the addition of new section 11A to entitle firemen to carry and use arms in the course of implementation of their functions, duties or powers conferred to it under this Act. The aim of this amendment is to enhance the security of Fire and Rescue Force infrastructures and personnel.

The Part further proposes to amend section 13 with the view to enhance the penalty and ensure that it is up-to-date and deters the commission of the offence prescribed.

Section 14 is proposed to be amended so as to distinguish the appointing authority for senior officers and other officers of the Force in order to make better provision regarding their appointment, promotion, confirmation and other administrative matters. Section 19 is proposed to be amended so as to empower Commissioner-General of the Force to make orders for the general governance of the Force.

This Part further proposes amendment of section 22 by compelling an owner or operator to provide fire safety protection in a building of twelve meters and above, above the level of the street or ground surface. The purpose of these amendments is to widen the scope of fire safety protection in buildings. Amendments are proposed in section 27 to provide for compensation for firemen and voluntary firefighters injured or who die in the cause of provision of services under this Act.

The Bill also proposes amendment in the Act by adding sections 31A and 31B introducing a general penalty and compounding of offences respectively. The objectives of the amendments are to facilitate better administration of offences and facilitate amicable settlement and discouragement of lengthy court trial process. Section 32 is proposed amended by adding matters which the Minister may make regulations for in respect of auxiliary fire units and fire dealers. The purpose of this amendment is to make provisions for supervision and control of the private and public fire and rescue service providers in Mainland Tanzania.

Part III proposes consequential amendments to the Police Force, Immigration and Prison Service Commission Act (Cap. 241) and the Employment and Labour Relations Act (Cap. 366), whereby various interpretation of terms are amended in the view to provide for their intended meaning to be in line with the Fire and Rescue Force Act, Cap. 427. The amendment further propose to incorporate members of the Fire and Rescue Force into the Commission.

This Part also proposes amend the Employment and Labour Relations Act so as to include Fire and Rescue Force in a list of exempted Forces from whom the application of the Employment and Labour Relations Act shall not apply.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura ya 427 kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika katika Sheria hiyo wakati wa utekelezaji wake pamoja na kufanya marekebisho katika sheria nyingine ili ziendane na

marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura 427, ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Kifungu cha 5 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuboresha mfumo wa utunzaji wa taarifa ya huduma zinazotolewa kwa mfumo wa kanzi data.

Inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 11A ili kuwapa Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haki ya kutumia silaha wakati wa utekelezaji wa majukumu, wajibu na mamlaka yao yaliyoainishwa chini ya Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha usalama wa miundombinu ya Jeshi, maafisa na askari.

Marekebisho pia yanapendekezwa katika kifungu cha 13 kwa kuongeza adhabu ili iendane na wakati na hivyo kuzuia utendaji wa makosa. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa yaliyoainishwa katika sheria.

Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutenganisha mamlaka ya ajira ya maafisa waandamizi na maafisa wengine wa jeshi kwa lengo la kuweka utaratibu bora kuhusu uteuzi, kupandishwa vyeo, kuthibitishwa kazini na masuala mengine ya kiutawala ya maofisa wa jeshi. Aidha, kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa mamlaka Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutengeneza amri za usimamizi wa jumla wa Jeshi.

Kifungu cha 22 kinarekebishwa kwa kumtaka mmiliki au msimamizi wa jengo kufunga mfumo wa vifaa vya moto kwenye jengo hilo. Vilevile marekebisho katika kifungu hiki yanaweka sharti kwa mtu yeyote anayekusudia kujenga jengo lenye urefu wa kuanzia mita kumi na mbili kutoka usawa wa ardhi kuwasilisha mchoro wa ujenzi wa jengo kwa Jeshi la Zimamoto kwa ajili ya ukaguzi na ushauri wa kiusalama kuhusu

masuala ya moto kabla ya kuanza kwa shughuli za ujenzi. Aidha, marekebisho yanapendekezwa kufanyika katika kifungu cha 27 kwa kutoa fidia kwa askari wa Jeshi la Zimamoto na watu wanaojitolea ambao hujeruhiwa au kufariki wakati wa kupambana dhidi ya majanga ya moto.

Muswada pia unapendekeza marekebisho katika Sheria kwa kuongeza vifungu vya 31A na 31B kwa kuweka adhabu ya jumla na ufililishaji wa makosa. Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha utaratibu wa utoaji adhabu na kupunguza mlolongo mrefu wa mashauri mahakamani. Vilevile kifungu cha 32 kinarekebishwa ili kuongeza wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kutunga kanuni ili kuzisimamia kampuni binafsi saidizi zinazotoa huduma za zimamoto na uokoaji.

Sehemu ya Tatu inapendekeza marekebisho yatokanayo katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza (Sura ya 241) na Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi (Sura ya 366), kwa kuboresha tafsiri mbalimbali katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza ili ziendane na marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Vilevile marekebisho katika Sheria hii yanakusudia kujumuisha wajumbe kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenda Tume. Aidha, Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366 inarekebishwa kwa lengo la kulijumuisha Jeshi la Zimamoto katika orodha ambayo masharti ya Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi hayatatumika.

Dodoma,<br>18 Agosti, 2021

GEORGE B. SIMBACHAWENE<br>*Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi*

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY THE HON. GEORGE B. SIMBACHAWENE THE MMINISTER OF HOME AFFAIRS AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE FIRE AND RESCUE FORCE (AMENDMENT) ACT, 2021"**

*(Made under S.O. 99(10))*

The Bill entitled "The Fire and Rescue Force (Amendment) Act, 2021" is amended as follows:

**A:** In Clause 10 by deleting the words "five hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings" appearing in the proposed section 31A and substituting for them the words "two hundred thousand shillings but not exceeding three hundred thousand shillings".

Dodoma,
......................, 2021

**GBS**
*MHA*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na kwa kweli imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa George Simbachawene kwa kuwasilisha vizuri sana hoja yako na kama tulivyosema, imeungwa mkono.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe Musa Azzan Zungu. Tafadhali Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu uwasilishe hotuba yako.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendment) Act, 2021).*

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendment) Act, No.2 of 2021).*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force (Amendment) Act, (No.2) of 2021)* ulisomwa Bungeni kwa Mara ya kwanza tarehe 31 Agosti, 2021 wakati wa Kikao cha kwanza cha Mkutano wa Nne.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge

uliuleta Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliujadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kupokea maoni ya wadau. Kamati ilipima na kubaini umuhimu wa maoni ya Wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na kuwa Muswada huu uliwasilishwa kwa Hati ya Dharura. Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mwaliko wa wadau ulitolewa ambapo jumla ya watendaji watatu kutoka Taasisi ya *Tangible Initiatives for Local Development* walifika mbele ya Kamati tarehe 2 Septemba, 2021 kwa ajili ya kuwasilisha maoni yao. Aidha, wadau tisa kutoka Taasisi ya Makampuni ya Ulinzi Binafsi (*Tanzania Security Industry Association)* na mdau binafsi mmoja, walitoa maoni yao kwa njia ya Maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wadau wetu wote kwa ushiriki wao pamoja na maoni yao yenye tija ambayo yameiwezesha Kamati kupambanua masuala ya msingi katika kuchambua na kushauri ipasavyo kuhusu maeneo mbalimbali yenye kuhitaji maboresho kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada. Mantiki ya Maudhui ya Marekebisho yanayopendekezwa; kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa, naomba kubainisha kwa ufupi maudhui ya marekebisho yanayopendekezwa na Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura 427, ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya neno "mzimamoto" lililotumika katika Sheria ili kutofautisha kati ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na mzimamoto mwingine kwa kuwa askari wote wa Jeshi la

Zimamoto na Uokoaji ni wazimamoto, lakini wazimamoto wote siyo Askari wa Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, Muswada pia unapendekeza marekebisho ya kifungu cha 5(2) cha Sheria ili kuboresha mfumo wa utunzaji wa taarifa ya huduma zinazotolewa kwa mfumo wa kanzidata na kurahisisha upatikanaji wa takwimu za matukio na kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kujipanga kimkakati katika kuboresha huduma zake.

Mheshimiwa Spika, vilevile Muswada katika Ibara ya 5, unapendekeza kufanya marekebisho na kuongeza kifungu kipya cha 11A ili kuwapa Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haki ya kutumia silaha wakati wa utekelezaji wa majukumu, wajibu na mamlaka yao yaliyoainishwa chini ya Sheria hii. Kamati ilijiridhisha kuwa, kwa kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni miongoni mwa Majeshi yaliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto ikiwemo askari kujeruhiwa, wizi na uharibifu wa miundombinu *(fire hydrants)*, marekebisho haya ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, hii itawezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuimarisha usalama wa miundombinu yake ikiwa ni pamoja na ofisi na magari ya zimamoto, usalama wa Maafisa na Askari hususan wakati wa matukio ya moto, kuzuia wizi kwenye majengo na maeneo ambayo yamekutwa na matukio ya moto, vilevile kuliwezesha Jeshi kutumia silaha hizo katika mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilijiridhisha kuwa uzoefu wa kumiliki silaha upo katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania Zanzibar na vilevile katika nchi za Afrika za Algeria, Misri, Morocco na Msumbiji. Aidha, makampuni ya ulinzi binafsi yanayotekeleza shughuli za kuzima moto hubeba silaha wakati wa matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha 13(3) yanakusudia kuongeza adhabu

kutoka faini isiyozidi shilingi laki mbili hadi kufikia faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja. Kamati imejiridhisha kuwa adhabu hii itasaidia kuwafanya wananchi kutambua umuhimu wa kuilinda miundombinu ya kuzimia moto *(fire hydrants)*. Aidha, Kamati inaona kuwa adhabu hii inalingana na madhara ambayo yanasababishwa na kushindwa kuzima moto kutokana na uharibifu uliofanywa na watu. Hii itasaidia kuhakikisha udhibiti wa majanga ya moto kupatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kuwa miundombinu *(hydrants)* mingi imeshaharibiwa kwa kujua au kutokujua, Kamati imesisitiza kuwa adhabu inayopendekezwa na marekebisho ya sheria hii isiziguse taasisi au wananchi walioharibu miundombinu hiyo kabla ya sheria hii kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 14(3) kwa lengo la kuweka utaratibu bora kuhusu uteuzi, kupandishwa vyeo, kuthibitishwa kazini na masuala mengine ya Maafisa wa Jeshi kwa Mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi ya Polisi, Magereza na Uhamiaji. Suala hili ni jema ili kuweka utaratibu bora katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, vile vile marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha 19 yanampa uwezo Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuzingatia amri na maelekezo ya Waziri, kutengeneza amri na miongozo ya usimamizi wa jumla wa Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza kurekebisha kifungu cha 22(1) kwa kumtaka mmiliki au mwendeshaji wa jengo kuwajibika kufunga mfumo wa vifaa vya moto *(automatic fire sprinklers)* kwenye jengo lenye urefu wa mita kumi na mbili (sawa na ghorofa tatu) na zaidi juu ya usawa wa ardhi ikilinganishwa na hapo awali ambapo sharti hili liligusa majengo kuanzia mita 24 sawa na ghorofa saba. Kamati ilijiridhisha kuwa vifaa hivyo vitaanza kuwekwa kwenye majengo yanayojengwa sasa, hata hivyo kwa majengo ya zamani msisitizo unawekwa kuwa vifaa vya

kung'amua moto *(fire detection system)* viwekwe. Hii ni kwa sababu ya faida za kiusalama kwa majengo hayo kukingwa na majanga na wananchi wanaoishi kuhakikishiwa usalama wao.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanapendekezwa pia katika kifungu kidogo cha (2) ili kumtaka mmiliki au mwendeshaji wa jengo lenye urefu wa kuanzia mita kumi na mbili juu ya usawa wa ardhi kuwasilisha kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji michoro ya ujenzi wa jengo kabla ya utolewaji wa kibali cha ujenzi. Hii inahusu majengo yote mapya yanayojengwa na yanayohitaji kupata kibali kupitia mamlaka ya Serikali za mitaa (TAMISEMI). Lengo ni kuwapatia wamiliki au wasimamizi ushauri wa kitaalam wa jinsi ya kujikinga na majanga ya moto na namna ya kusaidia uokoaji wakati wa hatari na hivyo kuongeza mawanda ya usalama wa moto kwenye majengo. Hata hivyo, Kamati inashauri marekebisho yataje wazi kuwa nyumba zinazokusudiwa ni zile zinazohitaji kibali cha TAMISEMI huku elimu zaidi ikiendelea kutolewa kwa wamiliki na wasimamizi wa majengo katika sehemu ambazo hazihitaji kibali hicho cha TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Muswada pia unapendekeza marekebisho katika sheria kwa kuongeza vifungu vya 31A na 31B kwa kuweka adhabu ya jumla na ufililishaji wa makosa, mtawalia. Malengo ya marekebisho hayo ni kuwezesha usuluhishi na kupunguza mlolongo mrefu wa mashauri Mahakamani pale inapobidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kuwa adhabu katika kifungu cha 31A inapendekezwa ili kujumuisha makosa ambayo hayana adhabu mahsusi katika Sheria kuu na Kanuni zake. Vilevile, adhabu inayopendekezwa katika kipengele 31B ni ile ambayo inatolewa pale ambapo mkosaji atakutwa ametenda kosa na kupewa nafasi ya aidha kukubali kosa na kulipa faini au kukubali kupelekwa Mahakamani kwa ridhaa yake.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 32A kuhusiana na

mamlaka ya Kamishna Jenerali ya kuandaa miongozo kwa ajili ya kampuni binafsi saidizi zinazotoa huduma ya zimamoto na uokoaji na mawakala wa uuzaji na usambazaji wa vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Kamati imejiridhisha kuwa suala hili ni jema kwa kuwa litawezesha usimamizi na udhibiti wa Kampuni binafsi zinazotoa huduma za zimamoto na uokoaji Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza marekebisho yatokanayo na Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza, Sura ya 241 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366, kwa kuboresha tafsiri mbalimbali katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza ili ziendane na marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Hii ni pamoja na kujumuisha Wajumbe kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenye Tume hiyo na kulijumuisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Orodha ya Vyombo vya Jeshi ambavyo masharti ya Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi hayatatumika kwa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kufanya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; matokeo ya kurekebisha Sheria inayokusudiwa ni pamoja na:-

(i) Kuondoa mgongano katika utekelezaji wa sheria;

(ii) Kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iii) Kuimarika kwa usalama wa maisha ya watu na mali zao dhidi ya moto na majanga mengine;

(iv) Kuimarisha usalama wa miundombinu, viongozi waandamizi, maafisa na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(v) Kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji zinazotolewa na kampuni binafsi; na

(vi) Kurekebishwa kwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza, Sura 241 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kama nilivyoeleza katika sehemu ya maudhui na uchambuzi wa Muswada, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho katika Muswada huu, kwa kuwa yana lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hiyo pamoja na kufanya marekebisho katika sheria nyingine ili ziendane na marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati wa uchambuzi, Kamati ilibaini jumla ya masuala ya msingi tisa na dosari moja ya kiuandishi na kiuchapaji, ambapo Kamati ilishauri ipasavyo na wakati wa kikao cha pamoja na Serikali cha tarehe 4 Septemba, 2021, Serikali ilitoa ufafanuzi wa kina kuhusu maeneo hayo na baadaye kufikia muafaka wa namna ya kuviweka vifungu hivyo ili kuleta tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo ya awali, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala mahsusi *(Special Issues);* Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 6(3)(b) inayopendekeza adhabu kwa mtu yoyote anayeharibu au kutumia miundombinu ya zimamoto kinyume cha taratibu iandikwe upya kwa kuonesha kuwa adhabu hii haitawagusa watu ama taasisi ambazo kwa namna moja au nyingine zimeathiri miundombinu ya zimamoto kabla ya sheria hii kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9(2) inayopendekeza mmiliki au msimamizi wa jengo lolote kupitisha ramani za majengo yake kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya ukaguzi na kupata ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya

zimamoto, kifafanuliwe ili kitaje mahsusi ni ramani za majengo yapi zitatakiwa kuwasilishwa badala ya kutumia neno *any building*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inayoongeza Kifungu 31A kinachopendekeza adhabu kwa makosa ambayo hayana adhabu mahsusi katika Sheria pamoja na Kanuni zake, adhabu hiyo iwe ni si chini ya shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tatu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inayoongeza kifungu 31B kinachopendekeza matumizi ya Kanuni kwenye kutoa adhabu katika makosa ya kufifilisha *(compounding)*, Kamati inaishauri kwa kuwa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura Na.1, kimeweka masharti ya Kanuni zinazotungwa chini ya sheria kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali, ni vyema Bunge likazipitia Kanuni hizo mapema iwezekanavyo kwa utaratibu uliopo ili kuepusha uwezekano wa matumizi mabaya ya vifungu hivyo. Hii ni pamoja na Kanuni zitakazoandaliwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Ibara ya 11(h), (i) na (k) ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, dosari za kiuandishi; pamoja na Kamati kubaini masuala ya msingi yenye kuhitaji maboresho ya Bunge lako Tukufu, pia ilibaini kuwa Ibara ya 17(c) inapendekeza kifungu kidogo cha (v) kwenye Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na wakati huo huo Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5, nao unaongeza kifungu kidogo cha (v) katika Sheria hiyo hiyo ya Ajira na Mahusiano Kazini. Naomba kutoa taarifa kuwa, Serikali imeliona suala hilo na kulifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa jumla; pamoja na ushauri wa Kamati uliotolewa hapo juu kuhusu masuala mahsusi ya kiuchambuzi yaliyobainika katika Muswada huu, pia kupitia majadiliano ya wadau pamoja na Serikali, Kamati iliweza kubaini masuala ya kuzingatiwa na Serikali wakati wa kutekeleza sheria hii kama ifuatavyo:-

(i) Elimu itolewe kwa wananchi na Taasisi kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, maeneo yote yenye miundombinu hiyo yatambuliwe kama Kifungu Na. 13 (1) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji (Sura ya 427), kinavyoelekeza, nanukuu: *"The Force shall provide and maintain, or cause to be provided and maintained, such fire hydrants and other water installations as are necessary for securing the best practical use of the available water supply in case of the outbreak of fire, subject to the approval of the relevant authority and the location of every such hydrant shall be plainly indicated by a notice or distinguishing mark or plate which may be placed on any wall or fence adjoining a street or public place."* Hii itawezesha wananchi kuyatambua maeneo yenye miundombinu ya zimamoto *(fire hydrants).*

(ii) Pamoja na kuwa Sheria hii inalenga majengo yote mapya yanayojengwa na yanayohitaji kupata kibali kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa kuwa madhara yatokanayo na ajali za moto ni makubwa, Kamati inashauri Serikali ihamasishe wamiliki wote wa majengo ambayo hayaguswi na sheria hii, kuwasilisha ramani zao kwa ajili ya ushauri wa kitaalam. Hii itasaidia kudhibiti majanga ya moto kwa urahisi katika maeneo ambayo hayajapimwa na hivyo kuimarisha usalama wa maisha ya watu na mali zao dhidi ya majanga ya moto.

(iii) Serikali iendelee kurasimisha ardhi kwa maeneo ambayo hayajapimwa ili kuwezesha maeneo mengi zaidi kufikiwa na huduma za zimamoto na uokoaji. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa madhara yatokanayo na ajali za moto.

(iv) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liwezeshwe kibajeti ili kufanikisha utekelezaji wenye tija wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili iweze kufanyia kazi jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Mbunge; Naibu Waziri, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Mbunge; Katibu Mkuu, Ndugu Christopher Kadio; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhan Kailima; pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu. Aidha namshukuru Ndugu Optat Mrina, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali *(CPD)* kwa ushirikiano wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wadau wetu wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao kwa ajili ya uboreshaji wa Muswada huu. Hakika, Kamati ilifaidika sana na maoni yao ambapo kwa kiasi kikubwa yaliwajengea uelewa zaidi Wajumbe katika kuchambua Muswada huu na kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa kuufanyia kazi Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge *(Hansard)* pamoja na taarifa yote hii inayowasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa Uongozi thabiti uliofanikisha uchambuzi wa Muswada huu na uratibu wa shughuli za Kamati hii. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald S. Magili na Wanasheria wa Bunge; Ndugu Agnes Ndumbati, Ndugu Nesta Kawamala na Ndugu Thomas Shawa.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati, Ndugu Ramadhan Abdallah, Bi. Grace

Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, wamefanya kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yote haya, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuukubali, kuujadili na kuupitisha Muswada huu kwa utekelezaji bora zaidi wa sheria hii na kwa manufaa mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI WA MWAKA 2021 *[THE FIRE AND RESCUE FORCE (AMENDMENT) ACT, 2021]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 ***[The Fire and Rescue Force (Amendment) Act, No.2 of 2021].***

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 ***[The Fire and Rescue Force (Amendment) Act, No.2 of 2021]*** ulisomwa Bungeni kwa Mara ya kwanza tarehe 31 Agosti, 2021 wakati wa Kikao cha kwanza cha Mkutano wa Nne.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge uliuleta Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge

lako tukufu kuwa Kamati iliujadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.1 ***Hatua ya kupokea Maoni ya Wadau***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipima na kubaini umuhimu wa maoni ya Wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na kuwa Muswada huu uliwasilishwa kwa hati ya Dharura. Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Mwaliko wa Wadau ulitolewa ambapo Jumla ya Watendaji watatu (3) kutoka Taasisi ya *Tangible Initiatives For Local Development (TIFLD)* walifika mbele ya Kamati tarehe 02 Septemba, 2021 kwa ajili ya kuwasilisha maoni yao. Aidha, Wadau tisa (9) kutoka Taasisi ya Makampuni ya Ulinzi Binafsi (*Tanzania Security Industry Association)* na Mdau binafsi mmoja, walitoa maoni yao kwa njia ya Maandishi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru wadau wetu wote kwa ushiriki wao pamoja na maoni yao yenye tija ambayo yameiwezesha Kamati kupambanua masuala ya msingi katika kuchambua na kushauri ipasavyo kuhusu maeneo mbalimbali yenye kuhitaji maboresho kwenye Muswada huu.

## 2.0 **UCHAMBUZI WA MUSWADA**

### 2.1 ***Mantiki ya Maudhui ya Marekebisho yanayopendekezwa***

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa, naomba kubainisha kwa ufupi maudhui ya marekebisho yanayopendekezwa na Muswada huu kama ifuatavyo:-

2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura 427, ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya neno “mzimamoto” lililotumika katika Sheria ili kutofautisha kati ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na mzimamoto mwingine kwa kuwa askari wote wa Jeshi la

Zimamoto na Uokoaji ni wazimamoto lakini wazimamoto wote siyo Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

2.1.2 **Mheshimiwa Spika**, Muswada pia unapendekeza marekebisho ya kifungu cha 5(2) cha Sheria ili kuboresha mfumo wa utunzaji wa taarifa ya huduma zinazotolewa kwa mfumo wa kanzi data na kurahisisha upatikanaji wa takwimu za matukio na kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kujipanga kimkakati katika kuboresha huduma zake.

2.1.3 **Mheshimiwa Spika**, vilevile Muswada (Ibara ya 5) unapendekeza kufanya marekebisho na kuongeza kifungu kipya cha 11A ili kuwapa Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haki ya kutumia silaha wakati wa utekelezaji wa majukumu, wajibu na mamlaka yao yaliyoainishwa chini ya Sheria hii.

Kamati ilijiridhisha kuwa kwa kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni miongoni mwa Majeshi yaliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto ikiwemo Askari kujeruhiwa, wizi na uharibifu wa miundombinu (fire hydrants), marekebisho haya ni muhimu. Hii itawezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuimarisha usalama wa miundombinu yake ikiwa ni pamoja na Ofisi na magari ya zimamoto, usalama wa Maafisa na Askari hususan wakati wa matukio ya moto, kuzuia wizi kwenye majengo na maeneo ambayo yamekutwa na matukio ya moto, vilevile kuliwezesha Jeshi kutumia silaha hizo katika mafunzo.

Kamati pia ilijiridhisha kuwa uzoefu wa kumiliki Silaha upo katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania Zanzibar na vilevile katika nchi za Afrika za Algeria, Misri, Morocco na Msumbiji. Aidha, Makampuni ya Ulinzi Binafsi yanayotekeleza shughuli za kuzima moto hubeba silaha wakati wa matukio hayo.

2.1.4 **Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha 13(3) yanakusudia kuongeza adhabu

kutoka faini isiyozidi shilingi laki mbili hadi kufikia faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyo zidi shilingi milioni moja. Kamati imejiridhisha kuwa Adhabu hii itasaidia kuwafanya wananchi kutambua umuhimu wa kuilinda miundombinu ya kuzimia moto (fire hydrant). Aidha, Kamati inaona kuwa adhabu hii inalingana na madhara ambayo yanasababishwa na kushindwa kuzima moto kutokana na uharibifu uliofanywa na watu. Hii itasaidia kuhakikisha udhibiti wa Majanga ya moto kupatikana kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kwa kuwa miundombinu (hydrants) mingi imeshaharibiwa kwa kujua au kutokujua, Kamati imesisitiza kuwa adhabu inayopendekezwa na Marekebisho ya Sheria hii isiziguse Taasisi au Wananchi walioharibu miundombinu hiyo kabla ya Sheria hii kupitishwa.

2.1.5 **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu pia unapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 14 katika kifungu kidogo cha (3) kwa lengo la kuweka utaratibu bora kuhusu uteuzi, kupandishwa vyeo, kuthibitishwa kazini na masuala mengine ya maofisa wa Jeshi kwa Mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi ya Polisi, Magereza na Uhamiaji. Suala hili ni jema ili kuweka utaratibu bora katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi.

2.1.6 **Mheshimiwa Spika**, Vilevile marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha 19 yanampa uwezo Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuzingatia amri na maelekezo ya Waziri, kutengeneza amri na miongozo ya usimamizi wa jumla wa Jeshi hilo.

2.1.7 **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu pia unapendekeza kurekebisha kifungu cha 22 katika kifungu kidogo cha (1) kwa kumtaka mmiliki au mwendeshaji wa jengo kuwajibika kufunga mfumo wa vifaa vya moto (automatic fire sprinklers) kwenye jengo lenye urefu wa mita kumi na mbili (sawa na ghorofa tatu) na zaidi juu ya usawa wa ardhi ikilinganishwa na hapo awali ambapo sharti hili liligusa majengo kuanzia mita 24 sawa na ghorofa saba.

Kamati ilijiridhisha kuwa vifaa hivyo vitaanza kuwekwa kwenye majengo yanayojengwa sasa, hata hivyo kwa majengo ya zamani msisitizo unawekwa kuwa vifaa vya kung'amua moto (fire detection system) viwekwe. Hii ni kwa sababu ya faida za kiusalama kwa majengo hayo kukingwa na majanga na wananchi wanaoishi kuhakikishiwa usalama wao.

2.1.8 **Mheshimiwa Spika**, Marekebisho yanapendekezwa pia katika kifungu kidogo cha (2) ili kumtaka mmiliki au mwendeshaji wa jengo lenye urefu wa kuanzia mita kumi na mbili juu ya usawa wa ardhi kuwasilisha kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji michoro ya ujenzi wa jengo kabla ya utolewaji wa kibali cha ujenzi. Hii inahusu majengo yote mapya yanayojengwa na yanayohitaji kupata kibali kupitia mamlaka ya Serikali za mitaa (TAMISEMI). Lengo ni kuwapatia wamiliki au wasimamizi ushauri wa kitaalamu wa jinsi ya kujikinga na majanga ya moto na namna ya kusaidia uokoaji wakati wa hatari na hivyo kuongeza mawanda ya usalama wa moto kwenye majengo.

Hata hivyo, Kamati inashauri Marekebisho yataje wazi kuwa nyumba zinazokusudiwa ni zile zinazohitaji kibali cha TAMISEMI huku elimu zaidi ikiendelewa kutolewa kwa wamiliki na wasimamizi wa majengo katika sehemu ambazo hazihitaji kibali hicho cha TAMISEMI.

2.1.9 **Mheshimiwa Spika**, Muswada pia unapendekeza marekebisho katika Sheria kwa kuongeza vifungu vya 31A na 31B kwa kuweka adhabu ya jumla na ufifishaji wa makosa, mtawalia. Malengo ya marekebisho hayo ni kuwezesha usuluhishi na kupunguza mlolongo mrefu wa mashauri Mahakamani pale inapobidi kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejiridhisha kuwa adhabu katika kifungu cha 31A inapendekezwa ili kujumuisha makosa ambayo hayana adhabu mahsusi katika Sheria kuu na Kanuni zake. Vilevile, Adhabu inayopendekezwa katika kipengele 31B ni ile ambayo inatolewa pale ambapo mkosaji atakutwa ametenda kosa na kupewa nafasi ya aidha kukubali kosa

na kulipa faini au kukubali kupelekwa mahakamani kwa ridhaa yake.

2.1.10 **Mheshimiwa Spika**, Muswada unapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 32A kuhusiana na mamlaka ya Kamishna Jenerali ya kuandaa miongozo kwa ajili ya kampuni binafsi saidizi zinazotoa huduma ya zimamoto na uokoaji na mawakala wa uuzaji na usambazaji wa vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Kamati imejiridhisha kuwa suala hili ni jema kwa kuwa litawezesha usimamizi na udhibiti wa Kampuni binafsi zinazotoa huduma za zimamoto na uokoaji Tanzania Bara.

2.1.11 **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu pia unapendekeza marekebisho yatokanayo katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza (Sura ya 241) na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Sura ya 366), kwa kuboresha Tafsiri mbalimbali katika Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza ili ziendane na Marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Hii ni pamoja na kujumuisha Wajumbe kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenye Tume hiyo, na kulijumuisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Orodha ya Vyombo vya Jeshi ambavyo masharti ya Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi hayatatumika kwa Vyombo hivyo.

### 2.2 *Matokeo ya kufanya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto Na Uokoaji*

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya kurekebisha Sheria inayokusudiwa ni pamoja na:-

(i) Kuondoa mgongano katika utekelezaji wa Sheria;

(ii) Kuimarika kwa utendaji na kuongeza ufanisi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iii) Kuimarika kwa usalama wa maisha ya watu na mali zao dhidi ya moto na majanga mengine;

(iv) Kuimarisha usalama wa miundombinu, Viongozi Waandamizi, Maafisa na Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(v) Kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji zinazotolewa na Kampuni Binafsi;

(vi) Kurekebishwa kwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza, Sura 241 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika sehemu ya Maudhui na uchambuzi wa Muswada, Kamati inakubaliana na mependekezo ya marekebisho katika Muswada huu, kwa kuwa yana lengo la kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo pamoja na kufanya marekebisho katika Sheria nyingine ili ziendane na Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, wakati wa uchambuzi, Kamati ilibaini **Jumla ya masuala ya msingi tisa (9) na dosari moja (1) ya kiuandishi na Kiuchapaji,** ambapo Kamati ilishauri ipasavyo na wakati wa Kikao cha pamoja na Serikali cha tarehe 4 Septemba, 2021, Serikali ilitoa ufafanuzi wa kina kuhusu maeneo hayo na baadae kufikia muafaka wa namna ya kuviweka vifungu hivyo ili kuleta tija iliyokusudiwa

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo ya awali, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

### 3.1 *Masuala Mahsusi (Special Issues)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

(i) Katika ibara ya 6 (3) (b) inayopendekeza adhabu kwa mtu yoyote anayeharibu au kutumia miundombinu ya zimamoto

kinyume cha taratibu iandikwe upya kwa kuonesha kuwa adhabu hii haitawagusa watu ama Taasisi ambazo kwa namna moja au nyingine zimeathiri miundombinu ya zimamoto kabla ya Sheria hii kuanza kutumika;

(ii) Ibara ya 9 (2) inayopendekeza mmiliki au msimamizi wa Jengo lolote kupitisha ramani za majengo yake kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya ukaguzi na kupata ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya zimamoto, kifafanuliwe ili kitaje mahsusi ni ramani za majengo yapi zitatakiwa kuwasilishwa badala ya kutumia neno 'any building';

(iii) Ibara ya 10 inayoongeza Kifungu 31A kinachopendekeza adhabu kwa makosa ambayo hayana adhabu mahsusi katika Sheria pamoja na Kanuni zake, adhabu hiyo iwe ni si chini ya Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi laki tatu;

(iv) Ibara ya 10 inayoongeza kifungu 31B kinachopendekeza matumizi ya Kanuni kwenye kutoa adhabu katika makosa ya kufifilisha (compounding), Kamati inaishauri kwa kuwa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, kimeweka masharti ya Kanuni zinazotungwa Chini ya Sheria kuwasilishwa Bungeni ndani ya Siku sita baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali, ni vyema Bunge likazipitia Kanuni hizo mapema iwezekanavyo kwa utaratibu uliopo ili kuepusha uwezekano wa Matumizi mabaya ya vifungu hivyo; Hii ni pamoja na Kanuni zitakazoandaliwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Ibara ya 11 (h) (i) na (k) ya Muswada huu.

### 3.2 ***Dosari za kiuandishi***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kubaini masuala ya msingi yenye kuhitaji maboresho ya Bunge lako Tukufu, pia ilibaini kuwa Ibara ya 17 (c) inapendekeza kifungu kidogo cha (v) kwenye Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na wakati huo huo Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5, nao unaongeza kifungu kidogo cha (v) katika Sheria hiyo hiyo ya Ajira na Mahusiano Kazini.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa Taarifa kuwa, Serikali imeliona suala hilo na kufanya marekebisho.

3.3 ***Maoni na Ushauri wa Jumla***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ushauri wa Kamati uliotolewa hapo juu kuhusu masuala mahsusi ya kiuchambuzi yaliyobainika katika Muswada huu, pia kupitia majadiliano ya Wadau pamoja na Serikali, Kamati iliweza kubaini masuala ya kuzingatiwa na Serikali wakati wa kutekeleza Sheria hii kama ifuatavyo:-

(i) Elimu itolewe kwa wananchi na Taasisi kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, maeneo yote yenye miundombinu hiyo yatambuliwe kama Kifungu namba 13 (1) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji (Sura ya 427), kinavyoelekeza, nanukuu '*The Force shall provide and maintain, or cause to be provided and maintained, such fire hydrants and other water installations as are necessary for securing the best practical use of the available water supply in case of the outbreak of fire, subject to the approval of the relevant authority and the location of evey such hydrant shall be plainly indicated by a notice or distinguishing mark or plate which may be placed on any wall or fence adjoining a street or public place, ...' ;* Hii itawezesha wananchi kuyatambua maeneo yenye miundombinu ya zimamoto (fire hydrants)

(ii) Pamoja na kuwa Sheria hii inalenga majengo yote mapya yanayojengwa na yanayohitaji kupata kibali kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa kuwa madhara yatokanayo na ajali za moto ni makubwa, Kamati inashauri Serikali ihamasishe wamiliki wote wa majengo ambayo hayaguswi na Sheria hii, kuwasilisha ramani zao kwa ajili ya ushauri wa kitaalam. Hii itasaidia kudhibiti majanga ya moto kwa urahisi katika maeneo ambayo hayajapimwa, na hivyo kuimarisha usalama wa maisha ya watu na mali zao dhidi ya majanga ya moto;

(iii) Serikali iendelee kurasimisha ardhi kwa maeneo ambayo hayajapimwa ili kuwezesha maeneo mengi zaidi kufikiwa na huduma za zimamoto na uokoaji. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa madhara yatokanayo na ajali za moto;

(iv) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liwezeshwe kibajeti ili kufanikisha utekelezaji wenye tija wa Sheria hii.

## 4.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili iweze kuufanyia kazi, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Kailima pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu. Aidha namshukuru Ndugu Optat Mrina Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) kwa ushirikiano wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru Wadau wetu wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao kwa ajili ya uboreshaji wa Muswada huo. Hakika, Kamati ilifaidika sana na maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yaliwajengea uelewa zaidi Wajumbe katika kuchambua Muswada huu na kushauri ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa kuufanyia kazi Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD)

pamoja na taarifa yote hii inayowasilisha maoni ya Kamati. Majina ya Wajumbe hao ni:-

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb. - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb. - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Janeth Mauris Masaburi, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb. - Mjumbe
8. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb. -Mjumbe
19. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb. -Mjumbe
20. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb. - Mjumbe
21. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb. - Mjumbe
22. Mhe. Emmanuel Godwin Kunambi, Mb. - Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa Uongozi thabiti uliofanikisha uchambuzi wa Muswada huu na uratibu wa shughuli za Kamati hii. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald S.Magili, na Wanasheria wa Bunge, Ndg. Agnes Ndumbati, Ndg. Nesta Kawamala na Ndg. Thomas Shawa.

Kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo yote hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuukubali, kuujadili na kuupitisha Muswada huu kwa utekelezaji bora zaidi wa sheria hii na kwa manufaa mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mussa Azzan Zungu, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,**
**ULINZI NA USALAMA**

6 SEPTEMBA, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, tunakushukuru sana kwa kutupitisha katika maoni ya Kamati yako; na kwa kweli, kwa kuupitia Muswada vizuri na kufika mahali ambapo mmeelewana kabisa na Serikali. Tunawashukuruni kwa uelewa kwa pande zote mbili, asanteni sana kwa kazi njema.

Sasa ni wakati wa uchangiaji. Mchangiaji wa kwanza awe Mheshimiwa Zahor Mohamed Haji, afuatiwe na Mheshimiwa Felister Deogratius Njau.

Mheshimiwa Zahor.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwanza kuishukuru Serikali na pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya na kubwa kuliko yote kuweza kufanya kazi kwa karibu sana na Kamati yetu, jambo ambalo limetufanya kuwa kitu kimoja kwa lengo na maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Muswada na nitazungumzia mambo matatu. La kwanza, tumekubaliana kwamba kwa mujibu wa Muswada huu, Jeshi

la Zimamoto sasa linakuwa jeshi kamili, kwa maana ya kwamba litaingia katika mlolongo wa kijeshi; litafuata kanuni na taratibu zote za kijeshi, wala siyo jeshi kwa maana ya jina. Kwa hiyo, wenzetu wataalamu wafanye kazi zao, wali-*train* jeshi hili liwe kama jeshi kamili na siyo kwa maana ya kuzima moto tu, lakini kwa maana ya kuwa Jeshi la Akiba wakati wote likihitajika litaendelea kuwa jeshi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo, kwa sababu, tumeliita "jeshi," maana yake ni kwamba, litatakiwa kufuata taratibu zote zikiwemo za mafunzo pamoja na kumiliki silaha. Kumiliki silaha ni kwa sababu, hatuwezi tukawa na jeshi ambalo linamiliki maji, lakini halimiliki silaha. Wenzetu hawa wanafanya kazi kubwa katika maeneo mbalimbali na mara nyingi changamoto zinatokea kwa sababu kwenye moto wako wanaoathirika, lakini wako wanaopenda athari itokee ili wao waweze kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako kwenye hili lione kwamba tumekubaliana kama Kamati na Serikali kwamba tuliwezeshe jeshi hili ili pamoja na kufanya kazi yao ya msingi ya kuhakikisha wanazuia moto, wanahakikisha wanatoa taaluma ya moto na pia waweze kufanya kazi ya kulinda mali wakati ambapo pia wanazima moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kulinda mali tu, kuhakikisha kwamba wanazuia uhalifu, lakini nao wenyewe wanajilinda, kwa sababu mara nyingi askari wetu hawa wanashambuliwa na wanaposhambuliwa wanakuwa hawana uwezo wa kujikinga wao wenyewe kama askari. Kwa hiyo, nashauri Bunge lako lisaidie hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo, naomba sana; na hili naomba wenzetu wa Jeshi la Polisi, tumekubaliana sasa vyombo vyote hivi vinafanya kazi kwa pamoja kwa maana ya Polisi, kwa maana ya Uhamiaji, kwa maana ya wenzetu hawa wa Jeshi la Zimamoto, wote wanakuwa kwenye *umbrella* moja. Ombi langu, waendelee

kufanya kazi kwa pamoja kwa sababu moja ya msingi, mara nyingi linapotokea tukio la moto wanaowahi kwenye tukio hili ni wenzetu wa Jeshi la Zimamoto, lakini mara nyingi inatokea kwamba, wenzetu wa Jeshi la Polisi wanachelewa ama kupata taarifa ama kufika kwenye eneo la tukio. Kwa hiyo, madhara yake yanakuwa makubwa kwa sababu watu wanavamia; wako watu wabaya na wako watu wema. Kwa hiyo, tatizo letu ni watu wabaya.

Mheshimiwa Spika, ombi langu sasa, mtandao wa mawasiliano kati ya Jeshi la Zimamoto na Jeshi la Polisi kwa sababu, wako chini ya *umbrella* moja, wawe kitu kimoja ili wapeane taarifa kwa pamoja. Anapotokea *fire* kama ni *advance* na mwenzetu wa polisi awe pale ili kusaidia kazi hii ya kulinda watu na mali zao. Tusiwaachie wenzetu wa Jeshi la Zimamoto tu kazi ile kwa sababu kazi yao kubwa na ya msingi ni kuhakikisha kwamba, wanazuia moto usitokee au wanazima moto pale maeneo ambayo janga limetokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu na ushauri wangu kwa wenzetu wa Jeshi la Polisi, wawe *faster* au wawe na haraka kwenye kutafuta taarifa au kuzipokea, kuzichakata na kuhakikisha kwamba wanafika kwenye eneo la tukio kama ambavyo wenzetu wa Jeshi la Kuzima Moto wamefika. Naomba sana hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuliko yote, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mwenyekiti wetu, kwamba tuliwezeshe jeshi letu hili liweze kufanya kazi zake kama inavyotakiwa ili tuweze kufanya kazi kubwa ya Serikali, kulinda raia wake, kulinda na mali zao na kuhakikisha kwamba wanaendelea kuishi kwa usalama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji. Nimeshakutaja Mheshimiwa Felista Deogratius Njau na utafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ambaye ametusimamia kwa weledi mkubwa katika Kamati yetu na kuhakikisha mambo haya yanakwenda vizuri. Naenda kwenye kile kipengele cha 9 *amendment* ya *section 22 (a)* ambacho kinaonesha moja kwa moja kwamba, kuna vigezo maalum ambavyo vinawekwa ili mtu aweze kufungiwa *fire hydrants.*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri aende mbali zaidi kwa sababu tumeona majanga ya moto yakienda kwenye mabweni ya watoto wetu, masoko makubwa, mabenki na kusababisha athari kubwa sana, lakini ukiangalia kwenye *level* hizo wanaweza wasifikie kwenye vigezo hivi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri itolewe elimu maalum na wale watu waweze kujilinda ili kuepukana na hasara itakayoweza kutokea; mali au watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia katika kipengele hiki ambapo Jeshi la Zimamoto limekuwa jeshi kamili kwa mujibu wa sheria. Tumeshuhudia uhalifu mkubwa wa kiwango kikubwa. Hata juzi tu Karikoo pale wakati soko linaungua huku vibaka wanaingia kwenye *ATM Machines* wanavunja wanachukua. Kwa hiyo, kitendo cha Jeshi la Zimamoto kupata silaha na kuweza kujilinda na kulinda mali za watu, ni kitendo ambacho kinatakiwa kiungwe mkono kwa sababu jeshi hili kuitwa jeshi bila silaha ni sawa na kibogoyo kupewa mfupa atafune. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu liridhie jeshi hili kupewa *instruments* zake zote ili liweze kusimama kama jeshi. Kwa sababu, *sometimes* wanawaona kama wako legelege, lakini nafikiri utaratibu utafuatwa ili jeshi hili likasimame imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mpaka hapo sitakuwa na mengi ya kusema zaidi ya kushukuru kwa nafasi hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda nilikutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura ya 427 kama Muswada ulivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri na mapendekezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niipongeze Serikali kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Ndani na pia kumpongeza Mwenyekiti na Kamati nzima ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Kwa kweli, jambo hili limekuwa ni jema na limekuja kwa wakati ambapo majanga ya moto yanachukua kasi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nilikuwa natazama wakati ndugu yangu Mheshimiwa Zahor anatoa ufafanuzi juu ya suala zima la kuwa jeshi kamili, maana zamani ilikuwa inajulikana kama Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, sasa ni Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri wenzetu wanaosimamia jeshi hili watazame changamoto moja kubwa ya kuitwa jeshi, tusitazame tu haja ya kuitwa jeshi. Vitendo vya matukio ya moto yanatokea halafu wanakwenda pale wakiwa hawana maji, siyo vitendo vya jeshi, ni vitendo vya kikosi. Sasa mnakwenda kwenye jeshi, ni lazima myaangalie mambo hayo. Hakuna jeshi linaweza likawa linafanya uzembe wa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujielekeza katika Kifungu Namba 11(a)...

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. Watu wengi wanashindwa kuelewa. Vyombo hivi vinapokwenda kuzima moto, vinakwenda vikiwa vimekamilika na vina maji ndani ya magari yao. Changamoto inapatikana, *pressure* inayotumika ku-*discharge* maji kwenye magari haya ni kubwa mno. Inachukua muda mchache sana maji yale kuweza kwisha na baadaye kuonekana gari imekuja bila maji. Ndiyo maana sheria hii sasa inaweka kipengele cha kulinda *fire hydrants* ambazo ndiyo sehemu sasa ya kuweza kupata *rescue* ya kuchukua maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo kwamba magari haya yanakwenda kuzima moto bila maji, hiyo, siyo kweli. Magari yanakwenda na maji na ukakamavu upo wa kutosha, tatizo yana-*discharge* maji kwa *pressure* kubwa yanakwisha upesi. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mwenyekiti nimeipokea ingawa haiendani na taarifa halisi zilizoko kwenye Umma wa Watanzania. Tunaarifiwa na vyombo vya Habari hivyo, nasi hatuendi kwenye matukio yote; na sijamsikia Mwenyekiti anasimama kupinga taarifa hizo za vyombo vya Habari. Kwa hiyo, haisaidii sana hapa Bungeni. Marekebisho haya ya sheria hayahusiani na hilo; hilo nilikuwa nimeweka tu kwamba, tunapozungumza jeshi, tutazame dhima ya jeshi badala ya ilivyokuwa kikosi.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hasa inaanzia kwenye Kifungu cha 11(a) ambacho kimeongezwa kwenye Muswada huu ambacho kinawapa nafasi sasa Askari wa Zimamoto kutumia silaha. Katika hoja hii, kutumia kwao silaha kumeelezwa humu kwenye Muswada huu kwamba ni kwa lengo la kulinda miundombinu ya jeshi ambayo ni hayo magari, sehemu za kuhifadhia maji na maeneo mengine. Sasa lazima niseme kwamba iwe wazi au iongezwe zaidi

kwamba hata kulinda mali za wananchi maeneo wanapokwenda kufanya uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki kilichoko kwenye Muswada kinazungumzia miundombinu ya jeshi. Kwamba, wanapewa silaha kwa ajili ya miundombinu ya jeshi. Nataka pale ikiwezekana waongeze, *"pamoja na kulinda mali katika maeneo yanayofanyiwa shughuli za ukoaji wa moto." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nilichangie katika hili ni suala la Kifungu Namba 22 ambacho kinataka sasa majengo yote yenye urefu kutoka usawa wa ardhi kwenda juu mita 12 yanayojengwa, michoro yake ipitishwe kwenye Jeshi la Zimamoto kwa ajili ya kuzingatiwa kwa vifaa vya zimamoto katika majengo hayo. Jambo hili naona ni jema na zuri, lakini kitu kimoja tu ambacho nataka niombe, tumekuwa na tatizo la urasimu katika ofisi zetu. Kuna watu wanataka kujenga majengo haya, watapeleka zimamoto, anaambiwa acha hapa, utarudi wiki ijayo uje uchukue. Huyu mtu anatakiwa aende Mipango Miji, anatakiwa aende kwa Bwana Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawazo yangu ambayo nataka kushauri ni kwamba, Jeshi hili la Zimamoto lihusike katika kuangalia mambo haya, lakini lihusike pale ambapo Kikao cha Kamati ya Mipango Miji kinapokaa kupitisha *building permit,* ndipo nao waalikwe kuhudhuria. Kwa sababu wakati mwingine kunatokea mpaka upotevu wa nyaraka. Unapeleka michoro yako ya jengo, unataka kwenda kuichukua, wanasema hiki hakionekani, hiki hakionekani kwa sababu, kimekaa muda mrefu kwenye ofisi mojawapo. Sasa wote wakutane kwenye Kikao cha Mipango Miji kinachotoa *building permit* watazame michoro hapo na wakubaliane au kutokukubaliana na mchoro huo wakiwa kwenye kikao cha pamoja badala ya mwananchi kuzunguka ofisi moja moja anatembeza nyaraka hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndio mambo ya msingi niliyoyaona.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. Mita 12 ndiyo ghorofa tatu? Mita 12!

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Kuanzia ghorofa tatu.

**SPIKA:** Inafika hapo eeh! Maana tusije tukasema mita 12 halafu kumbe ni hapa karibu karibu tu.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, kwenye sheria humu wamesema mita 12, hawakusema ghorofa ngapi.

**SPIKA:** Eeh, ndiyo nilikuwa najiuliza, maana kwenye taarifa ilisema ghorofa tatu. Nilikuwa nalinganisha hizo mita 12 na kilichoandikwa ghorofa tatu endapo ni inakaribiana. Kama inakaribiana, haya.

Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kuipongeza Kamati ya NUU kwa ushirikiano wao mzuri wakaweza kuufanya Muswada huu wa Sheria wa Jeshi la Zimamoto na Uokozi leo kuingia ukumbini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia Ibara ya 6(3)(b), kinazungumzia *fire hydrants.* Kwa kweli, jeshi limejipanga na mitaani tayari *fire hydrants* zipo, lakini haziwezi kuonekana na kwa bahati mbaya ziko katika mitaa ambayo wanaishi watu au wananchi wetu, lakini na ndimo mnamopatikana na majanga ya moto. Sasa kuwepo sehemu hizo siyo tatizo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililokuwepo hapa kuna sheria inaweza ikaja ikawazonga wakazi wa pale wakati watakapoharibu miundombinu hiyo. Wakati miundombinu

ile ipo wao hawaijui wala hawaifahamu ina maana uharibifu utatokea.

Mhwshimiwa Spika, sasa nilikuwa naliomba Jeshi la Zimamoto waanze kutoa elimu waweze kutembelea kila sehemu zilizokuwa na *Fire Hydrant* zao ili watoe mwongozo na maelekezo na waambiwe kwamba Sheria tayari ipo na adhabu itatolewa wao waliokuwepo kwenye mitaa waweze kulinda kwa sababu wakati ninapokwenda pale linapotokea janga la Moto *fire* zinapokwenda wanapoanza kuushambulia ule moto maji yakiisha ndio wanatumia maji yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa na pale ikiwa yale maji au mtu katoka na kioski chake kajenga pale kwenye *Fire Hydrant* wao watafika pale hawaoni kitu. Na kama pale hawaioni wanajua ipo mtu kaweka kioski chake watampa adhabu kumbe yule mtu kwa bahati mbaya hajui, hajapata elimu hajaelezwa. Kwa upande wangu ningependa hilo watoe elimu ili watu wazingatia elimu na wajue kwamba nitakapokwenda kinyume na hili adhabu itaniandama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia Ibara ya 5 kifungu cha 11(a) Ibara ya 5 ambayo inazungumzia kwamba Jeshi la zimamoto sasa hivi inatakiwa wawe na Silaha wawe na Amari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote ni haki yao kwa sasa kwa hali ya nchi inavyokwenda na upanuzi wa mitaa na miji. Wakati wanapokwenda kuzima moto, majanga ya moto yanapotokea kila mtu pale anakuwa na utashi wake wengine wanakwenda kuangalia, wengine wanakwenda kusaidia, wengine wanakwenda kwa kuiba na pale tuseme wao wanashughulikia kuzima moto huku watu wanashughulikia kuiba au wakati mwingine maji yamewaishia wanakwenda kwenye *fire hydrant* huku watu tayari wanaanza kuwashambulia. Sasa kwa vyovyote lazima wawe na kitu cha kuwalinda na pale hawalindwi wao tu kuna miundombinu yao wanawalinda na raia na mali zao kwa sababu nao watakuwepo.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine polisi wanawahi, wakati mwingine polisi wanakawia kufika lakini wao watakuwa tayari wapo wanaushambulia ule moto pamoja na kulinda mali za Serikali pamoja na kulinda na mali za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hii kujihami inawezekana hata wanapokuwa maofisini, unajua siku hizi anaweza akatokea mtu akaja akawaingilia tu ofisini kwao bila ya kutegemea anajua humu ndani kazi yao kulinda maji tu lakini anajua hapa nikiingia kwenye kikosi nikifanya fujo naweza kushughulikiwa wakati wowote kwa sababu wao tayari ni jeshi kamili wanastahili kuwa na silaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia Ibara ya 9, Ibara ya 9 inayopendekeza marekebisho ya kifungu cha 22 nakubaliana nao na maelezo yao kwamba lazima nyumba zinazoanzia ghorofa ya tatu kwenda na kuendelea ziwe tayari na sehemu ya zima moto, ziweze kujiwekea kinga yao na hata hizi nyumba nyingine za chini vile vile zitakuwa na utaratibu lazima lakini elimu ipite, waelekezwe wafahamishwe ili wajue kwamba hii ukiwa nayo itakusaidia wewe mwenyewe kama kinga yako ya kuweza kujikinga na madhara ya moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa nataka kuzungumzia kwamba kuna nyumba kuanzia ghorofa ya tatu mpaka kwenda juu kuendelea ambazo zilijengwa zamani hawa watakuwa vitu hivyo wengine hawana sasa wasiwachukulie kwenye sheria haraka haraka lazima wafanya utafiti wayapitia yale majengo wakawape elimu ili na wao hata kama wao walijenga zamani kwenye hii Sheria na wao itawagusa kama watakuwa vifaa hivyo hawana lakini wasiwachukuliwa sasa hivi Sheria imeshapita wao majengo yao hayana wakaweza kuwapa adhabu hilo litakuwa halipo sahihi kwa upande wao.

Mheshimwa Spika, na isitoshe kuna nyumba nyingine za ghorofa zipo sehemu za mitaani miundombinu yake ya tabu hata kama litatokea janga la moto kufika tabu tena

isiwe kuwa ndio sababu kwanini nyumba yako umeharibu na nyumba nyingine, wakati yeye alijenga zamani na yeye alipojenga hakuelewa nini kitafanyika halafu ikawa limetokea lililotokea kwa bahati mbaya mkamtia adhabu, lazima haya yaangaliwe na tuweze tuyafuatilia sisi kama Jeshi la Zimamoto na tuweze kulitekeleza kabla ya kumpa mtu adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiria kwa haya machache ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly, *no! no!* Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi nichangie kwenye Muswada huu nilikuwa na mambo matatu tu ya kuchangia. Kwanza kabla ya kutoa mawazo yangu nipongeze Jeshi la Zimamoto kwa kwa kazi nzuri inayofanywa ingawa inatakiwa waongeze juhudi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Tanzania Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya hasa wakati huu anafanya ile *royal tour* Mungu ambariki sana na amlinde na majanga yote wakati anafanya hiyo *royal tour* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niende *straight* kwenye mchango wangu sasa kwenye Muswada, kwenye kifungu cha 11 nimeona kuna makosa kidogo aidha sijui inawezekana ya uandishi wakati naupitia huu Muswada inawezekana kamati haikuona kwa sababu haikusema kwenye mapendekezo yake na pia haikuonekana. Lakini nimeona kwenye kifungu cha 11 cha Muswada kinaleta marekebisho kwenye kifungu cha 32 cha Sheria Mama, ambacho kifungu cha 32 cha Sheria Mama kina *Paragraph* (a)-(h), (h) ina *(i),*

Mheshimiwa Spika, kwenye marekebisho ilivyoletwa kwenye Muswada wanasema kinafanyiwa marekebisho

kifungu kwa kuondoa *paragraph* (h). Sasa haya marekebisho yanapofanywa ya kuondoa *Paragraph* (h) kifungu kidogo cha (b) kimesema kina *rename* kimetumia neno ku-*rename* kifungu cha (h) kuwa (n) na (o).

Mheshimiwa Spika, sasa wakati ninakipitia nimeona kama kime-*chopper numbering* kwa hiyo Mheshimiwa Waziri aiangalie vizuri ime-*chopper* maana yake kimeenda (n) na (o) hakijapita (m), na (h) mpaka (I) kipo kwenye marekebisho lakini kwenye sheria mama kuna *numbering* zimekosewa. kwa hiyo, unaweza kuiona hiyo Mheshimiwa Waziri wakati anapokuja kufanya majumuisho.

**SPIKA:** Endelea na linalofuata baada ya kuchangia nitakuomba uje hapa utakaa pembeni na Mheshimiwa Waziri au *AG* hapo mtaona hilo likoja.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN**: Mheshimiwa Spika, nimuoneshe.

**SPIKA:** Endelea na linalofuata na linalofuata.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN**:Mheshimiwa Spika, Sawa ahsante la pili nilitaka kuchangia ukisoma kwenye Sheria Mama hii sura ya 427 na Muswada unaoleta mapendekezo ya Sheria Mama hakuna sehemu nimeona Sheria zinatoa wajibu wa raia kulisaidia Jeshi la Zimamoto wakati wanafanya *operation* zao za kuzima moto hasa kwenye suala la *fire hydrant* ki-mantiki baadhi ya wakati Jeshi linapokwenda kufanya kazi ya kuzima moto hizo *hydrant* maana yake wao wanatumia maji kuzima moto na maji yanaweza yakawa yapo mbali, tuchukulie mfano moto unazimwa Dodoma Mjini na *Hydrant* pengine ipo Kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, alivyosema Mwenyekiti maji yakishamalizwa inabidi *fire* litoke kufuata maji kisasa lakini hapa kati kabla ya kufika Kisasa kwa mfano kwenye Sheli ya Shabiby panaweza pakawa pana magari ya maji ya *private* ambayo yanauza maji *private*, yakawa yanaweza ku-*rescuer*

*situation* kabla ya gari la *fire* kufika Kisasa ambapo mbali, hata wakirudi huku moto umeshateketeza.

Mheshimiwa Spika, sasa je, hakuna sehemu sheria inatoa wajibu wa kisheria kwa raia kwenye *situation* kama hiyo kuisaidia *fire* maji? Kwa hiyo, nikawa nimeona aidha kama haiwezekani sasa hivi kuwekwa kwenye Mswada Sheria inaweza ikaletwa kwenye kanuni wakati Waziri anafanya kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wenzetu wanapopata dharura kama hiyo mpaka nyumba za *private* kwa mfano zenye ma-*swimming pool* zinasaidia gari za *fire* kunyonya maji kwenye yale ma-*swimming pool* kwenda kusaidia kuzima moto, kwa sababu miundombinu yetu bado ni migumu hizo *hydrant* wanazosema zipo mbali na ni chache baadhi ya wakati unaweza ukamkuta mtu tu *private* anayo lakini kama haujamuwekea wajibu wa kisheria huwezi kuja kumwajibisha baadaye akikataa kukupa yale maji yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, aidha ingewekwa kwenye sheria au kanuni *responsibilities* au *duty* ya raia yeyote ambaye anaweza kuisaidia *fire* kupata maji wakati wa kutoa msaada wa kuzima moto huo ndio ulikuwa ushauri wangu wakati nasoma kwenye hii sikuona.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niipongeze kamati mimi sio mwanakamati lakini nataka niipongeze kamati kwenye pendekezo lao namba moja wamesema kwamba wameshauri kwanza Bunge liridhie lakini pia kwenye kifungu cha 6 wamependekeza kwamba hii sheria i-*act* kwenda mbele isirudi nyuma hiyo ni jambo zuri sana ambayo naipongeza kamati hilo wameliona kwamba ha o ambao sasa hivi hawana hiyo miundombinu na wameshajenga hayo majengo tusiwarejee kuwaadhibu kwasababu wao wakati wanajenga sheria ilikuwa haifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sheria ianze kwa kwenda mbele hiyo ni *observation* kubwa sana imefanya na kamati yako na niwapongeze sana, ingawa nimesema hapa

kwamba sio mwanakamati huo ndio ulikuwa mchango wangu. Naomba nitumie hii kumuonesha Mheshimiwa Waziri kwenye mpangilio huu wa vifungu, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan kwa mchango wako mzuri, ila sasa wakishachukua maji wa *swimming pool* yale sasa ili ku-*refill* ile *swimming pool* inatakiwa apate yale maji bure asiletewe tena bili ya maji maana maji yake yametumiwa kwa faida ya umma au sio, Waziri ataangalia jinsi ya kuweka ili iwe *win, win* au sio, Mheshimiwa Vita Kawawa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza naomba niungane mkono na Kamati kwa mapendekezo yote ambayo yametolewa naungana nayo mkono.

Pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake lakini pia kwa kukubali mapendekezo ya Kamati ya Muswada huu, naomba niende kwenye kifungu cha 6 cha Muswada ambao una-*amend* kifungu cha 13 katika ile *principal act* ambayo inataka kutoa adhabu kwa wale ambao watazichezea zile *hydrant*.

Mheshimiwa Spka, hii naungana nayo mkono kwasababu ni muhimu sana wananchi wafahamu umuhimu wa miundombinu hii ya maji ya kuzimia moto, hasa wakati inapotokea majanga kama yaliyotokea hivi karibuni Kariakoo, miundombinu mingi hizi *fire hydrant* zilikuwa hazionekani zilipo zimepotea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na adhabu iliyowekwa ili kuwakumbusha wananchi umuhimu wa hii *hydrant* lakini ninaishukuru sana Serikali katika kile *principle act* haikuondoa kile kifungu cha 13 (1) ambacho kinaleta wajibu kwa jeshi letu la *fire* la kutunza pia hizi *hydrant* zilizopo, kuweka tunasema kwamba *the force shall provide and maintain or course to be provided and maintain such fire Hydrants and other water installations,* huo ni wajibu kwa *fire* na wajibu

huu nao unahitaji gharama pia kwa jeshi letu la *Fire* kwa hiyo hapa leo kwakuwa tupo na Serikali inatusikiliza ushauri wangu kwa Serikali pia.

Mheshimiwa Spika, katika mipango yetu ya bajeti tuiangalie sana pia Jeshi la *Fire* kuipa fedha za ku-*maintain* na ku-*install* hivi *fire hydrants* lakini pia suala hili pia ni mtambuka miundombinu hii ya *fire hydrants* inaharibiwa bia wakati tunatengeneza barabara wenzetu wa *TARURA, TANROADS* wanaifukia kwa hiyo ni wajibu nao pia kutambua hii miundombinu hii inakuwepo...

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA**: Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita unapewa taarifa na Mheshimiwa Sophia.

## TAARIFA

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA**: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba ni kweli anachozungumza kwamba jeshi hili linahitaji Serikali iwekeze zaidi ni jeshi ambalo katika bajeti wanapoomba bajeti ni jeshi ambalo linapata chini ya kiwango cha bajeti walichoomba, na hata ukiangalia mavazi yao tu hawezi kuwa na ujasiri wa kufanya kazi kama Jeshi

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakuunga mkono kwamba Serikali ilitazame jeshi hili linapoitwa jeshi liwe kama majeshi mengine na hii Waziri husika nafikiri unahaja una watoto watatu hakikisha huyu mtoto wa tatu na yeye anakuwa kama wale watoto wengine wawili, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamishna *General* yupo anasikia, Mheshimiwa Sophia anasema hata ile *uniform* yenu ebu tafuteni nyingine mkishaitwa jeshi sasa mbadilike na kikosi mje kivingine Mheshimiwa Vita Kawawa unapokea taarifa hiyo (*Kicheko*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naipokea vizuri kabisa asilimia 100 taarifa hiyo, kwa maana ya kwamba miundombinu pia inaharibika kwa wenzetu wanapotengeneza barabara kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba wanapotengeneza barabara pia wawe wanawasiliana na *Fire* lakini pia na Mamlaka za kutengeneza maji.

Mheshimiwa Spika, leo hii zinapungua sana *Fire Hydrants,* kwa mfano Dar es Salaam pale, nitatoa mfano wa Dar es Salaam barabara kutoka Morocco mpaka Mwenge kuna *Fire Hydrant* mbili na pale kuna maghorofa yapo mengi na wameweka hizi wakati wanatengeneza barabara, lakini *Fire hydrant* mbili pale pana *not less than 3 kilometers* kutoka Morocco mpaka Mwenge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita samahani endelea kusimama hivi Makatibu Bungeni hapa kuna *Fire Hydrant* tusije tukaungua hapa. Mheshimiwa Vita endelea na mchango wako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ziko mbili kwamba kwa mujibu wataratibu kwamba kila hatua au mita 100 kunatakiwa kuwe na *Fire hydrants* kwa hiyo angalu pale kwenye kilometa 3 zingekuwa kama 10 hivi angalau zingesaidia, kwa hiyo ni muhimu sana kuwepo ndio maana ninasisitiza wenzetu wa Jeshi la Zimamoto waongezewe fedha kwa ajili ya kuweza kuziweka hizi na kuzi-*maintain* hizi *Fire Hydrants*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kusema kweli lingine lilikuwa kwanini ninaelezea pia suala hili la Jeshi la Zimamoto kuongezewa fedha kwa sababu moja wana upungufu pia wa rasilimali watu, lakini pia vifaa na mafunzo, tunalifanya kuwa jeshi kwa hiyo hatuna budi pia waongezewe rasilimali watu, waongezewe vifaa, miundombinu kama vile magari ya *Fire*, magari ya *Fire* toka mwaka 2007 ndio walipewa magari mapya toka nje leo hii wana magari hapa Dodoma hapa nadhani tuna gari moja la *Fire* hapa lingine sijui tuliazimishwa kutoka Iringa. Kwa hiyo,

yaani kuna haja kabisa mahsusi ya kuwekewa fedha za kununuliwa vifaa au miundombinu ya kuzima moto wenzetu hawa wa *Fire*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kusomesha wataalam wa *Fire* zaidi ili waweze kujua kazi yao vizuri vijana hao wengine wapya wanaopelekwa kwa hiyo tunaomba sana kwa sababu hapa sasa hivi tuna chuo pia cha *Fire* kinafundisha *basic* hatuna kile cha *advance courses* ambazo wanaweza wakawa wanapata utaalam wa kutosha kwa hiyo tusaidie Serikali iangalie maeneo hayo yote ya kuwapa elimu, rasilimaliwatu, lakini pia vifaa kwa ajili ya kuweza kusaidia katika maeneo ya uzimaji moto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda Mheshimiwa Zungu malizia baada ya hapo mtoa hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali vilevile nishukuru Wabunge waliochangia na Wabunge wa Kamati kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kweli *they deserve* kupongezwa kwa namna walivyoweza kushughulikia Muswada huu kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisemi mambo mengi kwa sababu mengi yameshasemwa niko sana katika Kanuni, sheria inasema Waziri akishatunga Kanuni zikishakuwa *tabled* kwenye Bunge *within six days* lazima ziwe zimeshawasilishwa Bungeni na Kamati Ndogo ya Sheria iweze kuzifanyia kazi. Niombe tu migogoro mingi mitaani katika nchi yetu sasa hivi inatokana na Kanuni kutokuwa rafiki kwa wananchi kwa gharama kubwa sana ambazo wananchi wanatozwa mfano ukaguzi wa vifaa vya *fire* katika majengo ya watu, kuna maeneo wanatozwa mpaka laki mbili mpaka laki tatu kwa mwaka ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunategemea hizi Kanuni zinapokuja Bungeni ,kwa sababu Bunge imekasimu madaraka kwa Wizara lazima Kamati hii ya Sheria Ndogo ihakikishe wanazipitia na kuweza kurudisha mrejesho kwa Serikali ili ziweze kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa sheria hii kama chombo hiki kitakuwa hakina bajeti ya kutosha sheria hii nayo itakuwa haina nguvu ya kufanya kazi. Gharama za vifaa vya zimamoto ni kubwa sana, kuna gari inauzwa mpaka bilioni mbili gari moja ya zimamoto. Kwa hiyo, upo umuhimu wa Serikali kutazama ni namna gani wanaweza kusaidia kuilea na kulibeba Jeshi hili ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mambo mengine lazima tuwe wazi tufunguke, Ujerumani *State of Hamburg* walishatoa *offer* kujenga *Fire Academy* hapa Tanzania na *Academy* hiyo haipo popote *South of Sahara,* tungeweza kupata wanafunzi kutoka maeneo mengi sana nchi jirani na sisi maeneo haya kuja kujifundisha na Serikali ingeweza kupata mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vitu kama hivi vikija vinakaliwa havifanyiwi kazi, kwa hiyo utakuta watu hawana *appetite* ya kufanya kazi sijui kwa sababu gani.

Kwa hiyo, naomba nitoe rai tu kwa Waziri na timu yake *offer* kama hizi zikija, kuna *offer* ya pale Mchicha - *TAZARA* Serikali ya Japan walitoa tu *condition* jengeni jengo tutawaletea magari, tutawaletea *training* tutawaletea na madawa ya vifaa vya kuzimia moto, mpaka leo lile jengo sasa hivi wamekaa pale vibaka na wahuni ambao wanafanya mambo ambayo siyo, yote haya ni kwa sababu bajeti hakuna. Hivyo, ninaiomba Serikali wajaribu kuwapa kipaumbele kwani moto ni janga ambalo halina hodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo na mimi nikushukuru sana kwa namna ulivyotuongoza na namna tunategemea utatuongoza katika siku za mbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa mtoa hoja karibu sana, hapo hapo tu inatosha ukitumia kama dakika 15 siyo mbaya.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niwashukuru Wabunge wote kwa michango mizuri ambayo inaboresha zaidi Muswada wetu ambao uko mbele yako. Kipekee sana ninashukuru maoni ya Kamati ambayo pamoja na yale ambayo tumeyafanya katika Kamati, pia wametueleza maeneo mengine muhimu ya kuzingatia nami niseme tu maoni ya Kamati yote ambayo wametoa katika taarifa yao tumeyapokea na tutayazingatia.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu kama walivyosema ni kweli lazima tuendelee kutoa elimu kwa sababu majanga ya moto yanaendana sambamba na maendeleo ya kiuchumi na uwekezaji. Kadri tunavyowekeza kwenye majengo marefu, kadri tunavyojielekeza kwenye majengo ya kisasa na kutumia umeme sana ndipo tunapopata majanga zaidi ya moto. Zamani huko ukisikia kibanda kimeungua shambani ni upepo ulivuma ikawa hivi basi, lakini kwa sasa ni majanga ambayo yanaambatana na hasara kubwa. Hivyo, elimu itaendelea kutolewa na tutazingatia sana maoni ya Kamati ambayo imetoa kwenye kamati lakini pia na Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa kwamba kimsingi sheria huwa hairudi nyuma sheria inaanzia pale ilipotungwa kwenda mbele na ni matakwa ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wasiwe na wasiwasi kwamba baada tu ya kutungwa sheria hii basi matakwa ya marekebisho haya yataanza moja kwa moja kuanza kwenda kuwagusa hata wale ambao walijenga nyumba zao kabla ya kutungwa kwa sheria hii hapana, sheria hai-*apply retrospective* sheria inaanzia pale ilipotungwa kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na adhabu zilizosemwa lakini ni pamoja na matakwa ya kuzingatiwa

katika majenzi, hakuna nyumba itakuwa *condemned* kwa sababu eti haina kitu fulani na kitu fulani lakini kubwa hapa ni kwamba majanga haya ya moto yanapotokea yanasababisha hasara kubwa, kwa hiyo hata kama hauguswi na sheria hii kuanzia hapa ilipofikia lakini kwa kuwa sasa tumeleta sheria na tuna utaalamu na tumeanzisha jeshi hili kamili, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji basi ujuzi ule wa Jeshi hili utumike katika kufanya kutoa ushauri na ili kuweza kuwasaidia wadau wetu wananchi pia na wawekezaji kuhakikisha kwamba wanafanya marekebisho kwenye majengo yao hata kama siyo lazima lakini kwa kweli ushauri wetu ni huo kwamba ikitokea janga ya moto kwenye majengo tusianze kulaumiana, ooh! kwamba kwa sababu hatukuguswa na sheria basi hatuwezi kufanya marekebisho ya kuweka ving'amua moto lakini pia kuweka matakwa ya mahitaji ya ushauri ya Kikosi cha Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumzia na hapa nimpongeze sana Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, pia Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda wamezungumza kwamba sasa Jeshi limeshakuwa Jeshi na kama limekuwa Jeshi basi liwe na tabia ya kijeshi na kwamba matukio yanapotokea tunataka tuone mabadiliko ya kwamba tumekwenda kwenye Jeshi na watu wako *active*. Kimsingi kuzima moto ni uwekezaji pia unatakiwa Jeshi hili tulipe vifaa tuwekeze uwekezaji mkubwa tusizungumzie tu kuzima na maji siku nyingine tuzungumzie kuzima kwa kutumia helikopta na vitu kama hivyo. Sasa haya yote yanahitaji uwekezaji na niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuliona hilo na kwa kuweza kushauri mambo ya kuzingatiwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, suala la kumiliki silaha limesemwa hapa ni kweli kwamba silaha hizi tutazitungia Kanuni hazitaanza tu hivi bila kuweka Kanuni nzuri. Kwa sababu tutashangaa kweli kumuona Askari wa Zimamoto hakuna tukio la moto hakuna hatari yoyote iliyopo katika mazingira yaliyopo halafu na yeye ana bunduki ameshika hivi anatembea nayo, italeta mgongano mkubwa sana lazima tueleze katika Kanuni kwamba bunduki itatumika wakati gani,

itaruhusiwa na nani, na nani anayeambatana katika tukio wakati wengine wameshika silaha za kuzima moto lazima kuwe kuna wengine ambao wana kazi ya kuwalinda hawa wanaofanya ile kazi. Kwa hiyo, siyo kwamba wote watakuwa na bunduki kunakuwa hakuna tofauti kati ya Polisi na Zimamoto, lakini silaha ya kwanza ya Askari wa Zimamoto na Uokoaji ni kuwa na zana za kufanyia kazi ya kuzima moto au kuokoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, silaha inalinda hawa wanaofanya lakini na mali zile zinazokwenda kuokolewa kwa sababu tumejifunza na kuona kwamba kunatokea uvamizi na watu wanapora vitu wakati wa matukio kama haya na Askari wetu wanakuwa wako katika eneo la tukio wanashindwa kudhibiti kwa sababu hawana vitu vinavyoweza kusababisha wananchi wakaogopa kusogea katika matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo limesemwa Mheshimiwa Njau amesisitiza kuhusu elimu kutolewa pia nimesahau Mheshimiwa Mohamed Haji amesisitiza vyombo hivi kufanyakazi kwa pamoja. Ni kweli hili jambo la msingi sana kama vyombo hivi vitakavyokuwa viko chini ya Wizara moja na vyote sasa vinakuwa Majeshi havitafanya kazi kwa ushirikiano basi itakuwa fujo. Kwa sababu wakati Jeshi la Zimamoto wanakwenda kuzima moto mawazo yao ni kuzima moto, ni lazima katika mawasiliano hayo hayo Jeshi la Polisi na lenyewe linatoka kuja sehemu ya tukio likija kulinda watu na mali zao, hili ni kweli lazima tuliweke vizuri katika utaratibu ili lisije likaleta mgongano. Wale wakasema bwana ninyi si mna kila kitu ninyi endeleeni tu huko nasi tunaendelea na shughuli zetu hapa! Ni kweli kabisa kwamba tutatengeneza utaratibu ambao vyombo hivi vitafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine limeguswa na ni hili la majengo ya mita 12, kupitisha michoro yao kwa Zimamoto ili ipate ithibati na ushauri wa kitaalam wa namna ya kujenga. Hili jambo utaliona kama ni la kawaida ukiona matatizo yanayotokea kwa mabweni kwa mfano, mtu anaamua kujenga tu bweni la shule anaweka watoto wetu mle ndani, hajapata ushauri na watoto wale wana matukio mengi ya

moto yanatokea huko, kimsingi kama wangepata ushauri Jeshi la Zimamoto ndiyo lenye utaalam wa kusema katika mchoro huu mnaotaka kujenga inatakiwa kuwe kuna milango minne kwa ukubwa wa jengo hili au kuwe kuna milango mitatu, uwekwe mwingine hapa mwingine uwekwe hapa.

Mheshimiwa Spika, utakuta pia hata nyumba zetu tunazojenga unajenga mimi najifungia kule *master bed room* kule umeji-*seal* kule kabisa, umeweka kabisa hakuna hata namna ya kujiokoa hata likitokea janga, lakini pia hujaweka ving'amuzi vya moto lakini hawa wataalam wetu hawa wana ujuzi wa kushauri kwamba katika mchoro wako huu hapa unapaswa kuwa na mlango, hapa unapaswa kuwa kuna dirisha kubwa, hapa unapaswa kuweka kitu hiki kwa sababu moto ukitokea utaweza kujiokoa kwa stahili hii.

Mheshimiwa Spika, hivyo matakwa haya pamoja na kwamba tumesema ni kwa ajili ya majengo marefu kupitisha ili kupata ithibati hii na ili uweze kupata *building permit* vyombo hivi vitashirikiana kwa sababu vyote ni vyombo vya Serikali, nasi katika Jeshi la Zimamoto itabidi tuweke utaratibu kama mtu anataka kupitishiwa fomu zake zile apitishiweje, zifanyweje, tutaweka utaratibu ambao hautakuwa na urasimu mkubwa ili kuondoa changamoto ambayo Waheshimiwa Wabunge wana wasiwasi nayo, lakini kubwa hapa ni ule ushauri utakaotolewa na chombo hiki kwa watu wanaowekeza na kupata hasara yanapotokea majanga.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fakharia Shomari amesema *fire hydrants* zipo lakini tunaelewa kwamba wananchi wengine wamejenga maeneo ambayo *fire hydrants* zilipaswa kuwepo na kwamba leo amesema wasije wakapata usumbufu sheria hii itakapoanza kutumika. Kama nilivyosema *generally,* Wabunge wengi mmezungumzia suala la elimu, elimu itaanza kwanza na baadaye kama ilivyo utaratibu sheria hii yetu inaendeshwa kwa Kanuni na huwezi kuchukua hatua yoyote ya kisheria kutokana na sheria hii ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na namna ya utendeji kazi wake

kama hujampelekea kwanza *notice* ya kwanza kuna (a), kuna (b), na (c) ambayo ndiyo inayokuja kusema sasa hapa tunaweza tukachukua hatua. Kwa hiyo kimsingi hapa kutakuwa kuna mengi yamezungumzwa na kama mtu hajafanya kwa maksudi na alifanya bila kujua, itajulikana na kusema ukweli hawawezi wakatendewa hayo na wasiwe na wasiwasi kwa sababu kama tulivyosema sheria kimsingi haitumiki kwa kurudi nyuma kabla ilipokuwa haijatungwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine limezungumziwa na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan ilikuwa ni hawa *Voluntary Fire Fighters,* kwenye marekebisho haya tumeweka hawa Zimamoto wa Kujitolea. Wazima moto wa kujitolea hawa wametajwa na wametambuliwa na sheria lakini eneo lingine amezungumzia juu ya *renumbering* ya ile *clause* 11(b) ni kweli alikuwa yuko sahihi, kulikuwa kuna makosa ambayo tumeyaona na *Attorney General* anaona namna atakavyofanya.

Mheshimiwa Vita Kawawa amezungumzia kuiongezea bajeti Jeshi la Zimamoto ili kuweza kufanyakazi yake vizuri na kwa ufanisi, hili ni kweli na wote waliosema hilo nakubaliana nao, kusema kweli ili kuweza kufanya *fire hydrants* hizi ziweze kufanyakazi zake vizuri lazima kushirikiana na taasisi zingine za maji lakini na taasisi za Majiji au Halmashauri kwa pamoja ndiyo tuweze kufanya vizuri na hii imesemwa hata katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu pia amezungumzia kuwepo kwa Kanuni na Kanuni hizi zitakapotungwa basi zifanyike haraka na ziletwe Bungeni, hili tulikubaliana hata kwenye Kamati kwamba Kanuni hizi zitakapotungwa tunajaribu kushauriana ili tuweze kutengeneza Kanuni nzuri zitakazofanya sheria hii itekelezeke bila kuwa na changamoto za usumbufu lakini pia tulete ufanisi na kuepusha majanga ya moto hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi kwa kweli hayo ndiyo nimeona Waheshimiwa Wabunge wamechangia na

ninawashukuru sana wote waliochangia na wengine ambao hawakuchangia na wote tunawashukuru kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa kuhitimisha hoja yako vizuri.

Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 (*The Fire and Rescue Force (Amendments) Bill, 2021)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu sasa tuendelee.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Ukurasa wa Pili.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 11

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali sijui ndiyo hapa ambapo Kilumbe Ng'enda aliongea sijui ni wapi? Mheshimiwa AG

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndiyo Kifungu au Ibara ya Muswada ambayo Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan amesema kina mapungufu ya kiuandishi au kasoro ya kiuandishi Kifungu kidogo cha (b), ambacho badala ya kusomeka *renaming paragraphs (h) and (i) as paragraphs (n) and (o)* kinatakiwa kisomeke *renaming paragraphs* (h) and (i) *as paragraphs (m) and (n)* sasa hapa nimefanya *consultation* na Mwandishi Mkuu wa Sheria akanihakikishia kwamba kwa sababu hiki hakihusu *substantive issue* ni kurekebisha tu uandishi inatosheleza kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimama na kumjulisha Mwenyekiti kwamba tumeiona kasoro hiyo na tunaridhia kufanya marekebisho hayo isomeke *renaming paragraphs (h) and (i) as paragraphs* (m) *and* (n) na kwa rekodi za *Hansard* za Bunge itakuwa imetosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Kifungu cha 11

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa!

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebishoya Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2021 (*The Fire and Rescue Force Amendment Act, 2021),* Ibara kwa Ibara na kukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2021 *(The Fire and Rescue Force Amendment Act, 2021)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa, sasa Waheshimiwa Wabunge kazi yangu ni kuendana na kanuni zinavyotaka katika hatua hii ambapo nitakwenda kuwahoji kuhusu Muswada wa Sheria

ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa mwaka 2021.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote kabisa wameafiki Muswada huu, Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika katika sheria hiyo wakati wa utekelezaji wake pamoja na kufanya marekebisho katika sheria nyingine ili ziendane na marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii *(A Bill for an Act to Amend the Fire and Rescue Act for the purposes of addressing the shortcomings observe during the implementation of the law and to effect Amendments to other Laws to be in line with the proposed changes).*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2021 (The Fire and Rescue Force Amendment Act, 2021) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa natangaza rasmi kwamba Muswada huu umeshapitishwa na Bunge katika hatua zake zote na sasa tutaupeleka mezani kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata baraka zake na itakapokuwa hivyo basi tutawajulisheni kwamba sasa umekuwa sheria kamili ya nchi.

Tunapenda kuwatakia kila la kheri ndugu zetu wa Jeshi la Zimamoto kwa kweli kwa jinsi ambavyo baada ya kuwa wameitumia sheria waliyokuwa nayo mwanzoni sasa marekeisho haya yanaenda kuwaweka katika mahali tofauti kabisa na tunaamini kabisa ufanisi wao utaongezeka,

utendaji kazi wao utakuwa bora zaidi na wananchi watapata huduma ambayo ni ya kutukuka zaidi.

Kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia matarajio ya wananchi ni makubwa kwa Jeshi hili muhimu sana, ukitazama hata kwenye mataifa makubwa ukitazama kwa mfano kule Marekani ile *September Eleven* ilivyotokea na jinsi ambavyo watu wa *fire* walifanya kazi kubwa sana, ni Jeshi ambalo linaheshimika sana kwa wenzetu kote huko duniani, linapewa heshima kubwa kabisa, kwa sababu watu wa *fire* ni watu ambao wanatoa maisha yao.

Waheshimiwa Wabunge, kupambana na moto siyo kitu rahisi ni kitu kigumu sana unajua moto ulivyo, mioto mingine ni mioto hatari kweli lakini wao wanakwenda wanapambana na moto hata wao wanaweza kuathirika wanaweza kupoteza Maisha na kadhalika. Kwa hiyo, Askari wetu hawa ni Askari muhimu sana sisi kama Bunge tumetekeleza wajibu wetu, tumeweka kila mazingira mazuri kwa ajili yao kuweza kufanyakazi nzuri tunawatakia kila la kheri kabisa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na timu yako yote pamoja na *AG* tunawashukuruni sana kwa kazi hii iliyotukuka.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bado naendelea tu kuwasihi na kuwasisitiza tuendelee kuchangamkia kuzielewa sheria zinazoletwa mbele yetu, ni kazi yetu kabisa kila moja wetu msirudi nyuma, msifanye nini, usiseme kwa sababu mimi hapana, wewe ndiyo mtunga sheria. Kwa hiyo, tujitahidi kuzisoma na kabla hujaisoma sheria ni vizuri kuanza na kule mwisho kuelewa kwanza sheria yenyewe nini madhumuni na sababu ya sheria hiyo. Zimeandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili kwa kila sheria pale mwisho pana madhumuni na sababu ya sheria hiyo, ukipitia yale madhumuni na sababu utaona sasa kule ndani kwanini kwenye kifungu fulani kuna jambo gani na kadhalika, naendelea kuwapa moyo sana Waheshimiwa Wabunge tushiriki.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutunga sheria kama ninavyosema siku zote narudia kila wakati, sheria haina

ushabiki, sheria ni sheria, kwa hiyo tunapotunga tutunge kitu kizuri ambacho hata siku ukiulizwa mbele ya safari kwa nini hiki kitu kiko hivi basi ni vizuri ukawa na maelezo kuliko kwamba ulikuwepo lakini hukujihusisha au hukuhusika bila sababu za msingi. Watanzania wanatutegemea chombo hiki kutunga sheria nzuri na tuwaahidi kwamba kazi hiyo tutaifanya na mpaka sasa tunakwenda vizuri kwa kweli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo kwa kuwa sasa kazi za siku ya leo zote zimekamilika tena kwa wakati, basi naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho Saa Nane kamili mchana.

*(Saa 11.05 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Septemba, 2021 Saa Nane Mchana)*